# Nipashe

Ijumaa Julai 2, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580629

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**TRA** yafuatilia asasi za kiraia kulipa kodi

UKURASA 3



**Wananchi** wavunja kilabu cha pombe kujenga zahanati

UKURASA 16



**Mbappe akataa mkataba mpya PSG**

UKURASA 20

# UPIGAJI

• **Ripoti** BoT yabaini malipo mara mbili kazi moja, utekelezaji miradi wafanywa nje ya bajeti... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea taarifa ya ukaguzi maalum inayohusu matumizi ya fedha zilizotolewa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kati ya mwezi Januari na Machi mwaka huu, kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**UHAKIKI MWINGINE WA SIMU WAJA**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile...

UKURASA WA 4

**TADB NA AGF KUINUA KILIMO KWA DOLA MIL. 20**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na African Guarantee...

UKURASA WA 7

**KORTI YABARIKI KUFUTWA DIWANI CCM KISA SI RAIA**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Kigoma imebariki uamuzi wa kutengua...


**W'biashara walalamikia kutozwa faini tofauti na kosa**

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store


# Gwajima aibua udanganyifu malipo ya matibabu NHIF

UKURASA 2




**MICHEZO** NINJA AREJEA KUIVAA SIMBA KESHO UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Gwajima aibua udanganyifu malipo ya matibabu NHIF

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameagiza hatua zichukuliwe kwa wahusika waliobainika kufanya udanganyifu wa madai na kusababisha ubadhirifu wa fedha za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Waziri Gwajima amesema wahusika hao wamebainishwa katika ripoti ya miaka mitatu aliyokabidhiwa na Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, huku akitaka utekelezaji wake uhusishe vyombo vyote vya kisheria na ripoti aipate Julai 30, mwaka huu.

Pia amenusa harufu ya upotevu wa fedha za makato za mfuko huo katika hospitali 28 za rufani za mikoa.

Dk. Gwajima alitoa kauli hiyo jana, alipokuwa akizindua Bodi mpya ya Wakurugenzi na Maadhimisho ya miaka 20 ya Mfuko huo. Kuhusu ripoti aliyokabidhiwa na Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, ya miaka mitatu, Dk. Gwajima alisema:

"Kuna makato ukifuatilia ni aina moja ya ubadhirifu, wizi, ile ripoti ambayo Mkurugenzi nilikuagiza ukaniletea ya ubadhirifu katika kipindi cha miaka mitatu... ule ubadhirifu haufai, watu wameghushi na ni mabilioni, sitaki hata kuyatamka, wale watu ni wezi."

"Niwape salamu zangu kupitia hadhara hii kwamba wanaofanya ubadhirifu kwenye mfuko huu ili walipwe malipo yasiyo halali, na salamu zimfike katika kona zote za nchi hii kwamba leo hii akae nyumbani kwake alale akitambua anafanya mpango wa kulipa fedha alizoiba... ripoti ipo Mwenyeketi ichukue, na awekewe mpango wa kuzilipa uwe uwajibikaji wa kisheria kwa sheria za vyombo vyote."

"Haiwezekani watu tuwasajilie vituo, taaluma halafu wanatuibia wanasema hilo shirika linakufa haipo hiyo, ripoti hiyo ifanyiwe kazi na kila mwanataaluma aliyehusika kusaini malipo hayo yasiyo halali kwa mujibu wa taarifa hiyo, atendewe haki yake kupitia bodi na mabaraza.

DK. Gwajima alisema: "Rais alishasema hatutaki fedha za dhuluma, kwa hiyo mnachezesha mchezo mnasema shirika linakufa, mimi naenda nao mzima mzima, mimi na wao, waje majeshi milioni mimi nawafyeka, tuwaondoe taaluma za afya waende huko wakasomee wizi." Aliagiza watu hao waandikiwe waanze kulipa na uwajibikaji wa kisheria ufanyike, na kwamba wataenda mbali na kuwanyang'anya leseni zao.

Alimwagiza Katibu Mkuu na Bodi kuwasilisha taarifa Julai 30, mwaka huu, namna walivyoshughulika na wabadhirifu hao kwa kushirikisha vyombo vyote waliodanganya madai na kukosea ujazaji fomu za madai NHIF.

Akizungumzia upotevu wa fedha za makato, waziri huyo alisema utafiti unaonyesha Sh. bilioni 2.4 ambazo ni makato yatokanayo NHIF ambayo yangezuilika na yamefanywa kwenye hospitali 28 za rufani za mikoa kwa miezi 18 licha ya kuwa na wasomi.

Alisema wale wanaoendelea na michezo ya kudhoofisha mifumo ili isifanye kazi wapelekwe kwenye mabaraza na bodi zao za kitaaluma.

Waziri huyo alisema mtu anaandika dawa haieleweki ni fedha inakatwa na kwamba watarudishwa mafunzo kwa vitendo kwa kuwa utafiti umebaini kuna watu wanakosea kujaza fomu za bima kwa makusudi.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akifurahia jambo na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, baada ya kuwasili katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa, jijini Paris, nchini Ufaransa juzi, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: OMR**

## Upigaji wafichuliwa BoT

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amepokea taarifa ya Ukaguzi Maalum kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) inayohusu matumizi ya fedha zilizotolewa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kati ya Januari na Machi mwaka huu.

Taarifa hiyo inatokana na agizo la Rais Samia la Machi 28, mwaka huu alipopokea Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2019/ 20.

Katika taarifa ya ukaguzi maalum ambayo Rais Samia alipokea jana, CAG, Charles Kichere, alisema ukaguzi uliofanyika umebaini fedha zilizotolewa BoT katika kipindi hicho zilifuata taratibu zote, isipokuwa baadhi ya malipo yaliyokuwa yanatoka Hazina Kuu kwenda katika taasisi mbalimbali za serikali yalibainika kuwa na upungufu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ikulu jana, upungufu huo unajumuisha baadhi ya taasisi kama vile Wakala wa Barabara (TANROADS) na Mamlaka ya Bandari (TPA) kufanya malipo mara mbili kwa kazi moja au kuchelewa kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya malipo ya kazi husika.

Vilevile, CAG Kichere alisema kumejitokeza upungufu ambapo baadhi ya makandarasi waliotoa huduma, kucheleweshewa malipo yao, hali inayosababisha madeni ya makandarasi kuwa makubwa kutokana na riba ambayo ni mzigo kwa serikali.

Upungufu mwingine ni pamoja na kuwapo kwa miradi ambayo haikupangwa na hivyo kufanya malipo nje ya Bajeti ya Serikali na hivyo kukiuka taratibu za nchi ikiwamo Sheria ya Bajeti.

Hata hivyo, taarifa ya Ikulu haikubainisha kiasi cha fedha kilichotolewa katika upungufu uliobainika BoT.

Machi 28, mwaka huu, Rais Samia baada ya kupokea Ripoti ya CAG Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma, aliagiza kufanyike ukaguzi maalum BoT kufuatilia fedha zote zilizotolewa katika kipindi cha miezi mitatu ya mwanzo wa mwaka huu.

Ingawa hazikuwekwa hadharani sababu za kufanyika kwa uchunguzi huo, tayari kipindi hicho kulikuwa na madai yaliyoenea katika mitandao mbalimbali ya kijamii kwamba kulifanyika uchotaji wa mabilioni BoT muda mfupi baada ya kufariki dunia kwa Rais John Magufuli.

Katika hatua nyingine, Rais Samia jana alipokea taarifa ya maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti mwakani kutoka kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa.

Dk. Chuwa alisema Sensa ya Mwaka 2022 itatumia teknolojia ya kisasa ya kidijitali chini ya mfumo ulipo wa serikali katika ngazi zote za utawala kwa pande zote za Muungano.

Alisema sensa ya majaribio itafanyika Agosti mwaka huu katika mikoa saba ya Tanzania Bara na Zanzibar.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe: 01/07/2021

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya kesho **IJUMAA** tarehe 02-07-2021 kampuni ya ***HAINAN INTERNATIONAL LTD*** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MBEZI LUIS** kuelekea **TEGETA "A",** gari hilo lenye namba za usajili: **T 175 DFN / T 168 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **18.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.82** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5** |

3. Njia itakayotumika: **MBEZI LUIS hadi TEGETA kupitia GOBA .** ***Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

116340302

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**


## Maelekezo ya ada kidato cha 5 haya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amepiga marufuku wakuu wa shule zote za serikali kutoza michango ya kujiunga na kidato cha tano zaidi ya Sh. 188,000.

Amesema mkuu yeyote wa shule atakayebainika kukiuka agizo hilo, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Ummy alitangaza katazo hilo jana alipofanya ziara katika Shule ya Sekondari Bihawana mkoani Dodoma kukagua utayari wa shule za serikali kupokea wanafunzi wa kidato cha tano mwaka 2021.

Alisema kiasi hicho kinajumuisha ada ya Sh. 70,000.

Waziri Ummy alisema wanafunzi waliochaguliwa kwa mwaka huu ni 87,663 kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika shule 476 na kutoa wito kwa wazazi ambao wataamua kuwapeleka watoto wao kwenye shule za binafsi kutoa taarifa kupitia mfumo, ili kutoa fursa kwa wengine.

Aidha, aliwataka wakuu wa shule kuandaa mazingira mazuri ya kupokea wanafunzi na kuwapo na mahitaji yote muhimu.

Aliwataka wanafunzi wa bweni kuripoti Julai 3 na wa kutwa Julai 5.

Kadhalika, alisema katika ajira mpya za walimu hivi karibuni hakuna shule itakayokosa mwalimu wa Fizikia wala Hisabati.

Alifafanua kuwa walimu wa Fizikia walioajiriwa ni 1,360 wakati shule ambazo hazikuwa na mwalimu ni 1,100 na walimu wa Hisabati walioajiriwa ni 459 wenye shahada na stashahada 140 wakati uhaba ulikuwa kwa shule 400.

# Wafanyabiashara walalamikia kutozwa faini tofauti na kosa

**Na Beatrice Shayo**

BAADHI ya wafanyabiashara wilayani Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, wamelalamikia ukaguzi wa leseni za biashara na kutozwa faini huku risiti ikionyesha makosa ya maegesho 'wrong parking' wakati kosa ni kutokuwa na leseni ya vinywaji vya vileo.

Aidha, wamedai faini hizo kukusanywa kwa mtutu wa bunduki na baadhi kukamatwa na kupelekwa kituo cha polisi walikolipia faini hizo na kupewa stakabadhi tofauti na kosa.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, mfanyabiashara eneo la Mlalakuwa, Gasto Temba, alisema alikamatwa saa 5:50 usiku akiwa dukani baada ya magari mawili kuegeshwa nje ya duka hilo kuuliza mhusika na kumtaka aonyeshe leseni ya vileo. Pia walimtaka awaeleza kama duka ni jipya na amepata namba ya mlipakodi.

"Waliniambia hawataki maneno mengi na kunitaka nipande kwenye gari kuelekea kituo cha polisi cha Mabatini. Wakasogea mbele wakamkamata mwingine, nilizunguka nao katika gari lao wakiendelea kukamata wengine na walivyofika kituoni wakaniambia nichague kulala au kulipa faini, nilikubali kulipa lakini stakabadhi niliyopewa haihusiani na kosa," alidai.

"Walinitaka nitoe laki nne kwa sababu sina leseni mbili, wakaniambia nilipe Sh. 200,000 kwani wakinipeleka kituo cha polisi nitatakiwa kulipa Sh. 400,000 kwa sababu sina leseni mbili ilinibidi nilipe hiyo faini na kunipatia risiti ya maegesho ambayo imeandikwa Sh. 20,000," alidai. Kwa mujibu wa Temba, siku iliyofuata akiwa dukani na wenzake waliulizana kuhusu faini hiyo na kubaini kila mmoja alitozwa kiwango chake na kuna waliotozwa Sh. 100,000.

"Hapa bado sijaelewa nasikia faini kwa watu ambao hatuna leseni ya vileo ni Sh. 100,000, lakini mimi wamenilipisha Sh. 200,000. Niliendа kulalamika Ofisi za Serikali za Mitaa," alidai.

Mfanyabiashara mwingine ambaye hakutaka kujata jina lake gazetini alisema, alifuatwa dukani kwake majira ya saa saba usiku na kumtaka alipe faini ya Sh. 200,000 kwa vile duka lake amechanganya na vilevi.

Alisema kwa mazingira yalivyokuwa magumu kila akizungumza waligoma kumsikiliza na kumtaka aingie kwenye gari kwa ajili ya kupelekwa Kituo cha Polisi cha Mabatini.

Alieleza kuwa baada ya kufika aliwekwa ndani pamoja na wafanyabiashara wengine ambao hawakuwa na hela ya kulipa faini ya Sh. 200,000.

"Ilikuwa ni siku ya Ijumaa niliyokamatwa usiku akaniambia usipolipa utaendelea kulala hadi Jumatatu kwa ajili ya kufikishwa mahakamani nikamwambia hiyo hela sina akanipunguzia hadi 120,000 bado nikamwambia sina akaniacha," alidai.

Alisema aliachiwa Juni 12, mwaka huu, majira ya mchana baada ya kutoa faini ya Sh.100,000 na hakupewa risiti.

Akizungumzia suala hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Mlalakuwa, Sulemani Masare, alisema alithibitisha kupokea malalamiko ya wafanyabiashara kadhaa wiki mbili zilizopita kuwa walifuatwa na maofisa biashara wakiwa na polisi majira ya saa tano usiku polisi wakiwa na silaha.

"Ukamataji huo haukuwa rafiki ni shuruti kwa jinsi wananchi walivyonieleza wengi wao walipelekwa polisi na kuwekwa mahabusu na wengine kutakiwa kulipa faini kwa viwango tofauti, lakini walipewa risiti za maegesho kwa kiwango cha Sh. 20,000 wakati wamelipa kati ya Sh. 100,000 hadi 200,000," alisema.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, wafanyabiashara hao walidai kuwa walioshindwa kulipa Sh. 200,000 hawakupewa risiti jambo linalotia shaka risiti zenyewe na kiwango cha faini na ukamataji. Alisema baada ya kupokea malalamiko hayo aliwasiliana na baadhi ya viongozi wa Wilaya ya Kinondoni na hadi sasa hajajibiwa, huku akishauri manispaa kutoa elimu zaidi kuliko kutumia mtutu wa bunduki kukamata walipa kodi.

Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songolo Mnyonge, alithibitisha kupokea malalamiko mengi na kwamba anayafanyia kazi baada ya kupatiwa taarifa kwa kuwa operesheni hiyo imeanzishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Kinondoni.

"Hii operesheni imefanyika katika maeneo mengi na nimepokea malalamiko mengi sana na subiri kupewa taarifa rasmi kwenye kikao kabla ya kutoa tamko," alisema.

Licha ya Nipashe kutafuta ukweli kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Kinondoni, Sipora Liana, haikupata ushirikiano.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akizungumza na Waziri Mkuu wa Burundi, Bunyoni Guillaume, wakati aliposhiriki katika maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa nchi ya Burundi, Viwanja vya Uhuru Boulevard, mjini Bujumbura jana, ikiwa ni ziara ya siku moja nchini humo. **PICHA: OWM**

# Polisi yatangaza vita dhidi ya vibaka

**Na Marco Maduhu,**

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limesema limejipanga kuwadhibiti vibaka mkoani humo, ambao wamekuwa wakijihusisha na matukio mbalimbali ya uhalifu, ikiwamo kwenye makazi ya watu.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alibainisha hayo jana alipozumgumza na waandishi wa habari.

Alisema kwa sasa matukio ya uhalifu makubwa yamepungua na kubaki ya vibaka ambayo nayo siyo mengi kama zamani, na kuwaonya vijana ambao wanajihusisha na vitendo hivyo waache mara moja.

"Zamani matukio ya vibaka mkoani Shinyanga yalikuwa yakitokea 50 kwa siku, lakini kwa sasa yamepungua na kutokea tukio moja na mimi ni mtu wa doria na nitakomesha uhalifu mkoani hapa," alisema Kyando.

"Nitazungumza na wenyeviti wa mitaa, vitongoji, vijiji na kuweka mkakati wa kufanya ulinzi shirikishi, ili kukomesha uhalifu Shinyanga na mji kuwa salama," aliongeza.

Aliwataka madereva bodaboda mkoani humo, kutii sheria na kuzingatia taa za usalama barabarani, ili kuepukana na ajali zisizo za lazima zitokanazo na uzembe.

Katika hatua nyingine, kamanda huyo aliwaahidi ushirikiano waandishi wa habari mkoani humo na kuwataka kuandika habari zao kwa weledi, ambazo hazitaleta taharuki kwa kufuata miiko na maadili ya taaluma yao.

# TRA yafuatilia asasi za kiraia kulipa kodi

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imesema itaendelea kufuatilia kwa karibu na kuondoa changamoto za kisheria na utendaji kwenye fedha zinazokuja kupitia azaki kwa kuwa pesa hizo ni za walipa kodi wa nchi nyingine.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, wakati akisoma hotuba ya Kamishna Mkuu katika mafunzo ya asasi za kiraia kuhusu kodi iliyoandaliwa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THDRC).

"Wengi mmelalamikia makato ya 'SDL', suala la kucheleweshwa au kutopewa hadhi ya kutolipa kodi pamoja na riba na 'penalty' (faini) kubwa katika marejesho yaliyochelewa kutokana na kwamba azaki hutegemea mzunguko wa hela za wahisani," alisema Kayombo.

Alisema TRA kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali wataendelea kushughulikia changamoto ili kuboresha mazingira ya ulipaji wa kodi kwa kundi hilo kwa kuwa wanatambua mchango mkubwa wa asasi na watetezi wa haki za binadamu kwenye pato la taifa.

Alizitaja kodi zinazolipwa na azaki kuwa ni kodi ya mshahara (PAYE), kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kodi ya zuio, ushuru wa stempu na kodi nyingine.

"Asasi za kiraia zimekuwa zikifanya manunuzi makubwa na pia kutoa huduma mbalimbali kama vile elimu, afya, utunzaji wa mazingira, utawala bora na shughuli zingine nyingi ambazo zinachangia maendeleo ya kitaifa kwa ujumla," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Kayombo, ripoti ya mwaka 2015 ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ilionyesha 78 ya mapato ya asasi yalitumika kufadhili shughuli za maendeleo ya watu kama vile kilimo, afya, elimu, maji na huduma zingine za kijamii.

Alisema sekta ya azaki imekuwa na mchango mkubwa katika kukuza maendeleo ya nchi na hasa katika kodi kutokana na kuongozwa na sheria na kusimamiwa na taasisi tofauti.

"Kupitia mkutano huu ningependa kutoa wito kwa wadau wote katika sekta ya asasi za Kiraia kuzingatia sheria hizi tuweze kujenga taifa kwa pamoja," alisisitiza Kayombo.

Alisema TRA inatambua kuwa walipa kodi wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wa sheria hizo na wanapokutana na taasisi za serikali zinazohusika na mapato.

Naye Mratibu THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema takribani asasi za kiraia 150 zinahudhuria mafunzo hayo kuelekea Siku ya Watetezi wa Haki za Binadamu leo.

Alisema changamoto iliyopo katika asasi hizo ni pamoja na uelewa mzuri kuhusu masuala ya kodi hususani kwa maofisa wa TRA katika utoaji wao wa elimu ya kodi kwa asasi hizo.

"Asasi za kiraia hazina fedha zake ni fedha za wahisani kama kuna madeni yaweze kuombewa msamaha riba na kodi ili waweze kulipa tunaomba TRA ikaongea na mamlaka zingine angalau Azaki kwa zile zilizokuwa zinadaiwa zikapewa muda fulani wa kulipa malimbikizo kama yapo bila kuwa na riba na faini," alisema Olengurumwa ambaye kitaaluma ni wakili.

# Uhakiki mwingine wa simu waja kisa kasi ya uhalifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amesema kutokana na uwapo wa wimbi la uhalifu wa mitandaoni, atatoa muda maalum kwa Watanzania kuhakiki na kusajili laini zao kwa alama za vidole.

Aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizindua tovuti ya wizara hiyo pamoja na mpango mkakati wa miaka mitano (2021/2026).

Ndugulile alisema atatoa maelekezo kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kufanya uhakiki na kuwataka Watanzania kila mmoja kufanya uhakiki kwa kuwa muda utatolewa na laini zisizo hakikiwa zitafungwa.

"Tuna changamoto za uhalifu wa mtandaoni hivyo niwaombe Watanzania mhakikishe mnahakiki laini mlizosajili na nitatoa maelekezo kwa TCRA kuhakikisha zoezi hili linafanyika na tutatoa muda maalum, hakikisheni mtu hamsajili mwenzake laini maana kufanya hivyo ni kosa," alisema Ndugulile.

Aliongeza kuwa serikali itachukua hatua zaidi kwa sababu wizi wa mtandaoni umekithiri.

Alibainisha kuwa mwezi huu wataanza kutoa elimu kwa umma kuhusu namna bora ya matumizi ya mtandao, hivyo kutoa wito kwa wananchi kutokubali kugawa namba za simu kwa watu wasiowajua kwakuwa ni kinyume cha sheria.

Awali, Dk. Ndugulile alisema wizara hiyo imejipanga kuhakikisha kwa miaka mitano inajenga uchumi wa kidigitali.

Alisema katika kipindi hicho wanaenda kuboresha mkongo wa taifa kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano, ili yaweze kufika katika wilaya zote nchini pamoja na nchi jirani.

Alibainisha kuwa Serikali kupitia Shirika la Posta ina mpango wa kuikuza vizuri na kuirasimisha ili watu waweze kufanya biashara vizuri pamoja na uboreshaji wa anuani za makazi.

"Tunataka kila nyumba kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Idara za mipango miji, Tamisemi na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuhakikisha tunaweka mipango miji mizuri kwa kuboresha barabara mitaa na namba za nyumba," alisema Ndugulile.

Kadhalika, alisema serikali itabadili sheria ili kufuta tozo mbalimbali zinazokwamisha ubunifu wa vijana.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk.Zainabu Chaula alisema mkakati huo una maeneo sita, kwamba maandalizi yake yamechukua miezi sita kupitia kikosi kazi maalum kilichohusisha watendaji mbalimbali wa Wizara.

# TADB na AGF kuinua kilimo kwa dola mil. 20

**Na Beatrice Moses**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na African Guarantee Fund (AGF), wametiliana randama ya makubaliano yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 20 kwa ajili ya kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kwa wakulima wadogo, kati na wakubwa.

Akizungumza baada ya utilianaji saini wa makubaliano hayo jijini Dar es Salaam jana, Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamwaja, alisema yatakuwa chachu katika utekelezaji wa mpango wa tatu wa Taifa wa Maendeleo.


"Kwa niaba ya serikali, napongeza makubaliano haya kwani ni hatua kubwa kwa TADB kwa ushirika wao mkubwa na AGF, kwani utachochea maendeleo na ukuaji wa sekta ya kilimo hususani kwa kinamama," alisema Dk. Mwamwaja.

Alisema makubaliano hayo kwa kiasi kikubwa yatasaidia kuondoa changamoto ya dhamana katika benki nchini, hivyo kuwezesha upatikanaji wa mikopo hiyo na kuwawezesha Watanzania wengi kushiriki katika sekta ya kilimo.

"Watanzania wamekuwa wakikosa dhamana ya kupata mikopo kwenye benki zetu... makubaliano haya yanaenda kuleta ahueni kwa Watanzania walio wengi, ambapo wamekuwa hawana dhamana, hivyo kuwafanya washiriki kikamilifu kwenye sekta hii inayoajiri Watanzania zaidi ya asilimia 65," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa AGF, Jules Ngankam, alisema makubaliano hayo yamelenga kuongeza tija na kuifanya sekta ya kilimo itiliwe maanani zaidi ili kufikia maendeleo ya juu Tanzania na Afrika kwa ujumla.

"TADB imekuwa benki muhimu sana kwa kuwa ni mahsusi kwa shughuli za kilimo tu, hivyo tunaamini makubaliano haya yatasaidia kuifanya sekta ya kilimo ipige hatua na kutoa mchango mkubwa zaidi ndani ya Afrika," alisema Ngankam.




Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Temeke, Josephita Kinyondo (kulia), akitoa maelezo kwa wananchi waliofika kupata huduma kwenye Mahakama inayotembea wakati wa Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea kwenye viwanja vya Julius Nyerere, barabara ya Kilwa, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mahakama inayotembea yaamua mashauri 1,208

**Na Joseph Mwendapole**

MAHAKAMA inayotembea 'mobile court' imefanikiwa kusikiliza na kumaliza mashauri 1,208 huku watu 13,668 wakinufaika na huduma zinazotolewa na mahakama hiyo tangu ianzishwe.

Hayo yalisemwa jana na Hakimu Mkazi ambaye ni Mratibu wa mahakama hiyo, Moses Ndelwa, katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Alisema idadi hiyo ya mashauri na wanufaika wa huduma hizo ni tangu kuanza kutolewa rasmi kwa huduma hiyo Julai, 2019 hadi kufikia mwezi Mei, 2021 na kwamba mpango wa mahakama ni kupanua huduma hiyo.

Alisema mahakama hiyo imeongeza mafanikio katika mikoa miwili ya Dar es Salaam na Mwanza na imesikiliza na kumaliza mashauri hayo na kwa Mwanza pekee mashauri 520 yalifunguliwa na kumalizika katika kipindi hicho.

Vilevile, alisema usikilizwaji wa mashauri katika mahakama inayotembea ni wa haraka na yote husikilizwa na kumalizika ndani ya siku 30.

Naye Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mwanza, Monica Ndyekobora, alitoa wito kwa wananchi wa mkoa huo kuendelea kuitumia mahakama hiyo kwa kuwa mwitikio wa kufungua mashauri bado si mkubwa.

"Mahakama inayotembea imesaidia kupunguza mrundikano wa mashauri, hivyo ni rai yangu kwa wananchi wa mkoa huu kujitokeza kutumia Mahakama hii endapo wana kesi za kufungua kwa sababu inawapunguzia gharama wananchi, inatoa haki kwa wakati," alisema Ndyekobora.

Naye Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo-Mkuyuni ambaye anafanyakazi katika Mahakama inayotembea, Jenipher Nkwabi, alisema mashauri yanayofunguliwa kwa wingi katika mahakama hiyo ni ya ndoa na talaka.


Alisema kwa upande wa Mwanza hususani eneo la Mkolani/Buhongwa, kumekuwa na mwitikio mkubwa wa wananchi kutumia mahakama hiyo na kwamba Dar es Salaam hutoa huduma zake maeneo mbalimbali kwa nyakati tofauti.

Mahakama inayotembea ilizinduliwa rasmi Februari 06, 2019 katika sherehe za kilele cha maadhimisho ya Siku ya Sheria Nchini na aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Hayati John Pombe Magufuli.

## TANGAZO

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
## WAKALA YA BARABARA TANZANIA

# SALAMU ZA RAMBIRAMBI




**Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa TANROADS tumepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Kiongozi na Mpendwa wetu ENG. PATRICK MFUGALE kilichotokea tarehe 29 Juni, 2021 katika Hospitali ya Benjamin Mkapa Jijini Dodoma.**

**Hakika Tutakukumbuka Daima kwa Uongozi wako Mahiri, Uchapakazi uliotukuka, Weledi na Uzalendo wako kwa Taifa Letu.**

## PUMZIKA KWA AMANI MPENDWA WETU.

www.tanroads.go.tz

***MIUNDOMBINU BORA YA BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE KWA MAENDELEO YA TAIFA***

## MAONI & UCHAMBUZI

**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

# *Magereza isikilizwe wito kupunguza msongamano*

**JESHI** la Magereza limesema limeanza ujenzi wa magereza mapya na ngome kwenye magereza ya zamani, ili kukabiliana na msongamano wa mahabusu na wafungwa katika maeneo hayo.

Aidha, limesema kuna upungufu wa magereza katika wilaya 46 na tayari wamepata maeneo katika wilaya 26 kuwa na maeneo ya kuhifadhi watu hao.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Jeshi la Magereza nchini, Seleman Mzee, fedha za kazi hiyo ipo ingawa hakutaja kiasi, na wataendelea kuimarisha ili kuhakikisha wanaondokana na msongamano.

Alidokeza kuwa jitihada za Rais katika kutoa msamaha kwa wafungwa kumesaidia kupunguza idadi ya wafungwa, na sasa anaziomba mamlaka nyingine kama Polisi, Mahakama na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), kutimiza wajibu wao kikamilifu ili kupunguza msongamano.

Tatizo la msongamano wa wafungwa ni kubwa na limezungumzwa mara nyingi na aliyekuwa Rais wa awamu wa tano, Hayati John Magufuli, mara kadhaa alieleza nia ya kupunguza msongamano kwenye magereza.

Jambo hili ni tatizo kubwa hadi sasa na kuna jitihada zinafanywa na Ofisi ya DPP kwa kumaliza kesi kwa kufuta au kuondoa nia ya kuendelea na shauri husika, jambo ambalo linapunguza mahabusu.

Lakini wito wa Kamishna huyo ni muhimu kuzingatiwa na mamlaka nyingine ili kusaidia kuanzia polisi kufanya upelelezi kikamilifu, ili wanaofikishwa kwa DPP kwa ajili ya kupelekwa mahakamani wawe ni wahusika.

Vivyo hivyo, DPP naye afanye kazi yake kikamilifu kuangalia kama kuna kesi ya kujibu na kama ushahidi upo wa kutosha, ili kuepusha kuwa na watu wenye kesi za kawaida wanaosota ndani kwa muda mrefu na kuongeza mahabusu.

Ikiwa kutakuwa na ushirikiano au kila mamlaka kuwajibika ni wazi msongamano utapungua na magereza yatapumua, kutakuwa na hali bora maeneo hayo.

Uwapo wa mahabusu ni gharama kwa nchi kwa kuwa wafanyakazi wanaowalinda wanalipwa mishahara, marupurupu na mahitaji mengine, kulipa ankara mbalimbali za maji, umeme na majitaka pia kuwalisha, mavazi na viatu.

Licha ya magereza kutakiwa kujitegemea kwa maana ya chakula na mahitaji mengine kwa wafungwa kufanyakazi za uzalishaji bado hawajaweza kwa asilimia 100, na wamejikuta wanategemea fedha za serikali.

Lakini kwa mujibu wa sheria, mahabusu hawaruhusiwi kufanyakazi na hata wakifanya wanalindwa sana, jambo ambalo ni gharama sana, maana yake unakuwa na idadi kubwa ya watu wanaogharamiwa na kodi za Watanzania.

Lazima kuwe na mkakati wa kupunguza mahabusu kuanzia ngazi ya jamii, viongozi wa dini na mamlaka nyinginezo, vinginevyo ni kuendelea kubeba mzigo mkubwa wa kuhifadhi watu hao.

Pia ni vyema kasi ya ujenzi wa magereza ikaongezeka kwa kuzingatia kuwa kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi kuna Watanzania zaidi ya milioni 55, na mwakani itakapofanyika sensa nyingine kuna uwezekano mkubwa wa idadi hiyo kuongezeka zaidi.

Jitihada za pamoja zinahitajika katika kuhakikisha msongamano kwenye magereza nchini unapungua na wale ambao ni wafungwa wakatumika kwenye uzalishaji kwa ajili ya kuliwezesha jeshi hilo kujiendesha kwa gharama zake zenyewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Machinga wameingiza kiasi hiki, waboreshewe masoko*

Na Sabato Kasika

**MWISHONI** mwa mwaka 2018, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, alitoa vitambulisho 670,000 kwa ajili ya machinga, ili kuwawekea mazingira rafiki ya kufanya biashara.

Pia lengo lingine la serikali lilikuwa kuwahakikisha wamachinga hao ambao tegemeo kubwa la watu wa hali ya chini, wafanye shughuli zao bila kusumbuliwa.

Katika mchakato huo, kila mkuu wa mkoa alipewa vitambulisho 25,000, huku kila mjasiriamali mdogo akitakiwa kulipia kitambulisho chake Sh. 20,000 ambapo kiasi hicho cha fedha kilitakiwa kupelekwa TRA.

Kila mkuu wa mkoa alitakiwa kukusanya Sh. milioni 500 zinazotokana na gharama za vitambulisho hivyo, lakini yule ambaye mkoa wake unahitaji vingine zaidi aagize ili kuhakikisha kila mjasiriamali anakuwa nacho.

Mchakato wa kugawa vitambulisho hivyo umeendelea kuwapo ili kuhakikisha kundi hilo linachangia katika uchumi wa taifa kupitia vitambulisho hivyo, ambavyo kila kimoja gharama yake ni Sh. 20,000.

Tangu Rais wa awamu ya tano alipozindua utoaji wa vitambulisho hivyo kwa lengo la kuwatambua wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo, inaelezwa kuwa serikali imefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 46.71.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ameahirisha Bunge na kutoa ufafanuzi kuhusu vitambulisho na kuongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021, serikali iliamua kuboresha vitambulisho hivyo kwa kuweka picha na jina la mjasiriamali ili kuongeza udhibiti.

Lengo la kuviboresha ni kuwawezesha wajasiriamali kutumia vitambulisho hivyo kupata huduma za kibenki na bima ya afya na Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) itaendelea na utaratibu wa kusajili wajasiriamali hao kwa kutumia mfumo, kuchapisha vitambulisho na kuvisambaza kwa halmashauri husika ili vigawiwe.

Kimsingi, hatua hizo zinazochukuliwa na serikali kwa ajili ya wamachinga, ni nzuri hasa kwa kuzingatia kwamba nao wana mchango kwenye maendeleo ya nchi yao kutokana na kodi wanazolipa.

Lakini, ingependeza zaidi iwapo hatua zaidi zingechukuliwa kwa kuwatengenea maeneo rasmi ya kufanyia kuliko ilivyo sasa wametapakaa mitaani na kufanya biashara hata katika maeneo ambayo ni hatari.

Binafsi, ninaamini kwamba, kuwawekea mazingira rafiki ya kufanyia biashara ni pamoja na kuwatengea maeneo au masoko yao badala ya kuwaacha wakivamia vituo vya daladala, pembezoni mwa barabara au chini ya nyaya za umeme mkubwa hali ambayo si salama kwao.

Kwa wakazi wa jijini Dar es Salaam, watakuwa wameshuhudia jinsi ambavyo wafanyabiashara wadogo wakiwamo mama lishe, baba lishe, wauza matunda, mitumba na vitu vingine vidogo walivyozagaa.

Baadhi ya madai yao, ni kwamba hawajatengewa maeneo ya kufanyia biashara, au kama yapo, bado hayajaboreshwa, hivyo hawawezi kwenda kufanya shughuli zao katika mazingira ambayo si rafiki kwao.

Hadi sasa baadhi ya masoko hayana maji, vyoo na pia hayafikiki kirahisi, hali inayosababisha wakose wateja, hivyo wanaona ni bora waendelee kufanyia biashara kwenye maeneo hatari.

Lakini ikumbukwe mwaka 2016, Rais wa Dk. Magufuli aliwahi kuziagiza halmashauri kuhakikisha zinawatengea maeneo ya kufanyia biashara tena yakiwa yameboreshwa, ndipo wahamishwe.

Je, halmashauri zimeshindwa kuwatengea maeneo au masoko? Zimeshindwa kuboresha yaliyopo? Kwanini waendelee kuzagaa mitaani kana kwamba hawana umuhimu wakati zimekusanywa Sh. bilioni 46.71 kutoka kwao?

Kwa kuwa kundi hilo limetambuliwa na kupewa vitambulisho, ninadhani kuna haja sasa ya kuhakikisha linaacha kuhangaika huku na kule badala yake lisaidiwe kuwa katika maeneo rasmi.

Wapo baadhi ya wafanyabiashara wadogo ambao wamekuwa wakifanya biashara huku wakikimbizwa na wafanyakazi wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

Mfano hai upo, eneo la Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam, imekuwa kawaida kukuta wafanyabiashara wakihangaika kuwakwepa wafanyakazi wa TANROADS wasiwakamate.

Wataendelea na maisha ya aina hiyo hadi lini?

Kwa nini wahangaike kiasi hicho? Kwa nini wasitengewe maeneo yao ambayo ni rafiki kwa shughuli zao kuliko wanavyohangaika kila siku?

# Bomu lilivyoibua taharuki jirani Uwanja wa Ndege Dar

**Na Mary Geofrey**

TAHARUKI iliibuka juzi kwa abiria na wakazi walio jirani na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA), kufuatia jaribio la tishio la bomu katika jengo la pili la abiria katika uwanja huo.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini (TAA) kwa kushirikiana na JNIA walifanya jaribio hilo juzi asubuhi kwa lengo la kupima ufanisi wa mamlaka, kama wana uwezo wa kudhibiti tukio hilo.

Kufuatia tukio hilo, wakazi wa maeneo ya uwanja huo walipatwa na taharuki baada ya kuona magari ya kuzima moto, magari ya kubeba abiria na magari ya jeshi yakiingia na kutoka katika uwanja huo.

Abiria waliokuwa katika uwanja huo, walipatwa na mshtuko uliowalazimu kuanza kupiga simu kwa ndugu na jamaa wakiwaeleza kuhusiana na tukio hilo.

Baadhi ya abiria walionekana wakikimbia huku na kule, huku Askari wa Jeshi la Wananchi (JWTZ), Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, watumishi wa mamlaka hiyo wakiendelea kutoa huduma ya kwanza kwa abiria.

Akizungumzia tukio hilo, Kaimu Mkurugenzi wa JNN, Mhandisi Diana Munubi, alisema uendeshaji wa jaribio hilo ni wa siri na unajumuisha wadau wote na kwamba wanatumia kanuni na taratibu za kimataifa za mamlaka za viwanja vya ndege.

Alisema walishirikiana na wadau wote wa kiwanja hicho katika kufanya jaribio hilo, hali ambayo ilizuia taharuki na kuwafanya abiria kushindwa kuamini kama kweli ni jaribio.

Diana alisema kuna aina 13 za matishio ya kiusalama katika viwanja vya ndege yakiwamo mabomu ndani ya ndege na ndani ya uwanja, ndege kutekwa na uzuiaji wa hadhara kubwa wa kuingia maeneo ya vizuizi.

Alisema majaribio hayo yanatakiwa kufanyika kwa nadharia na asilia kama ambavyo wamefanya kwa siri bila ya wadau kufahamu.

Alisema majaribio kama hayo yanatakiwa kufanyika kwa nyakati tofauti kila baada ya miaka mitatu na kwamba wamekuwa wakizingatia utaratibu huo.

Mkuu wa Kitendo cha Usalama na Operesheni wa JNIA, Raymond Munuo, akizungumzia usalama wa mali za abiria, alisema wanatumia kamera zilizopo maeneo yote ya uwanja na mawakala wa ndege na watumishi wanaohusika na mali za abiria katika uwanja huo.

Alisema kumekuwapo na malalamiko ya wizi, lakini wamekuwa wakichunguza na kubaini haujafanyika katika eneo hilo la uwanja. Alisema wamekuwa wakiyadhibiti matukio hayo kwa kuendelea kuweka taratibu madhubuti zinazosaidia kuimarisha usalama wa abiria na mali zao.

# Mahakama yabariki kufutwa kwa udiwani kisa si raia wa Tanzania

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Kigoma imebariki uamuzi wa kutengua udiwani wa Ezekiel Mshindo kwa hoja kwamba hana sifa ya kushika nafasi hiyo kwa kuwa si raia wa Tanzania.

Uamuzi wa Mahakama hiyo ulitolewa Juni 28, mwaka huu, mbele ya Jaji Athumani Matuma baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili.

"Kama ripoti ya uhamiaji inasema mlalamikaji si raia na ripoti hiyo haijapingwa basi hakuna haja ya kutohalalisha au kuharibu uamuzi wa mlalamikiwa namba mbili na tatu kwa kutangaza kuwa kiti cha udiwani wazi kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa sababu mlalamikaji hana sifa, si raia," alisema.

Alisema Sheria ya Uchaguzi ya Serikali ya Mitaa inasema mtu atakuwa na sifa katika uchaguzi huo ikiwa atatimiza vigezo vya kuwa raia wa Tanzania. Mshindo alikuwa Diwani CCM alikuwa akilalamika dhidi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) , Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Ezekiel aliwasilisha maombi katika mahakama hiyo akipinga kuondolewa katika nafasi yake ya udiwani. Alikuwa diwani wa Kata ya Kagera - Nkanda, Kasulu na alishinda nafasi hiyo katika uchaguzi wa mwaka 2020.

Inadaiwa Aprili 14, mwaka huu, Katibu Mkuu wa TAMISEMI alimfahamisha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kasulu kuwa mmoja wa madiwani katika kata yake moja si raia wa Tanzania na kumweleza kwamba aanze kufanya mchakato wa uchaguzi ili kujaza nafasi hiyo.

Wakati wa usikilizwaji wa shauri hilo, Diwani alikuwa akitetewa na mawakili Fortunatus Muhalila, Ignatus Kagashe na Hamisi Kamilomilo na wajibu maombi walikuwa wakiwakilishwa na Wakili wa Serikali Allan Shija akisaidiana na Emmanuel Ladislaus.

Akiwasilisha hoja za mlalamikaji, Wakili Muhalila alidai kuwa kitendo cha kuitisha uchaguzi mpya kimefanyika isivyo halali kwa kuwa mteja wake alishakuwa diwani.

Alidai malalamiko ya kuwa si raia wa Tanzania ni ya kisiasa na hata mteja wake alipohojiwa na Idara ya Uhamiaji hakukubali hoja ya kwamba si raia pia hakupewa nafasi ya kusikilizwa katika ngazi ya kitaifa ya uhamiaji.

Katika hoja nyingine, Wakili Muhalila alidai ripoti ya Uhamiaji inajichanganya kwa kuwa ilikuwa ikizungumzia Yohana Mshita na mlalamikaji kwa wakati mmoja.

Alidai katika mazingira hayo haionyeshi ni yupi hasa anayezungumziwa kati ya mlalamikaji na Yohana, kwa msingi huo hiyo ripoti haina sifa ya kuwa kielelezo kwa upande wa wanadaiwa kinachoweza kuzingatiwa wakati wa kutoa uamuzi.

Mshindo anadai kupitia wakili wake kuwa jukumu la Mwenyekiti wa Halmashauri kumfahamisha Waziri kuhusu suala hilo lakini si jukumu la waziri kufanya hivyo kama inavyoonekana katika hiyo kesi, anaomba mahakama ione mchakato wote uliofanywa katika shauri hilo ni batili.

Akiwakilisha wajibu maombi, Wakili Shija alidai Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa haiwezi kuachiwa hasa inapotokea mabadiliko ya diwani kupoteza sifa kama ilivyotokea kwa mlalamikaji baada ya kubainika kuwa si raia wa Tanzania wakati wa uchaguzi.

Kuhusu mkanganyiko wa majina ya kata ya Kagera Nkinda na Kagera Nkanda, alidai huko ni kuteleza kwa karamu na haina uhusiano na hoja iliyopo kwamba mlalamikaji si raia wa Tanzania.

Kuhusu hoja mlalamikaji kutopewa nafasi ya kusikilizwa na Idara ya Uhamiaji, wakili huyo alidai alipewa nafasi ya kusikilizwa katika ngazi ya wilaya, kama ilivyoonyeshwa katika ripoti na mlalamikaji alipowasilisha nyaraka za utetezi wa uraia wake.

## NOTISI / TANGAZO

**MOPEH COMPANY LTD, MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD, CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD,** kwa mamlakatuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| NA | JINA LA MDAIWA | TAWI ALILOKOPA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | HILDA DOEGRATIUS MKAWE | ARUSHA | DOEGRATIUS MKAWE & HILDA DEOGRATIUS MKAWE | NYUMBA | KATA YA DARAJA MBILI MTAA WA NDARVOI | 17/07/2021 NA KUENDELEA |
| 2 | IGNAS NDELELIO KAAYA | ARUSHA | IGNAS NDELELIO KAAYA | NYUMBA | KITONGOJI CHA LOITA – HALMASHAURI YA MERU | 16/07/2021 NA KUENDELEA |
| 4 | ZUHURA IBRAHIMU GIWANA | ARUSHA | ZUHURA GIWANA | NYUMBA | KATA YA DARAJA MBILI MTAA WA ALINYANYA | 18/07/2021 NA KUENDELEA |
| 5 | FRANK PAUL ROIKA | ARUSHA | FRANK ROIKA | NYUMBA | KIJIJI CHA ENGORIKA KATA YA KIUTU | 19/07/2021 NA KUENDELEA |
| 6 | ERICK RIKOYAN LUKUMAY | ARUSHA | ERICK RIKOYAN LUKUMAY | NYUMBA | KIJIJI CHA OLORIEN KATA YA OLORIEN | 25/07/2021 NA KUENDELEA |
| 7 | KIPEJA TIMBER AND GENERAL SUPPLIES CO.LTD | MWANZA | JOHN TIMOTH PANGANI | NYUMBA YENYE HATI CT NO.50423,PLOT NO.800 BLOCK D IGOMA | KIKWETE/IGOMA | 16/07/2021 NA KUENDELEA |
| 8 | MARTHA JAMES SULULU | MWANZA | MARTHA JAMES SULULU | KIWANJA | IGOMBE | 17/07/2021 NA KUENDELEA |
| 9 | WILSON MASANGA GAMBA | MWANZA | WILSON MASANGA GAMBA | KIWANJA | NYAMHONGOLO | 19/07/2021 NA KUENDELEA |
| 10 | ABUU MOHAMED MASHAKA | MBEYA | ABUU MOHAMED MASHAKA | NYUMBA-PAGALA | RELINI UYOLE | 21/07/2021 NA KUENDELEA |
| 11 | GREEN USANGU ENTERPRISES | MBEYA | GREEN USANGU ENTERPRISES | NYUMBA | UYOLE | 22/07/2021 NA KUENDELEA |
| 12 | OBADIA HARUNA NKYEKYE | MBEYA | OBADIA HARUNA NKYEKYE | NYUMBA | MBALIZI | 25/07/2021 NA KUENDELEA |
| 13 | AMINA OMARY SAIDI | AGGREY | MOHAMED RAJABU NGULANGWA | NYUMBA | VIKINDU | 16/07/2021 NA KUENDELEA |
| 14 | GEDAPE LOGISTICS & GENERAL SUPPLY LTD | UKONGA | GEORGE JOSEPH YATERA | NYUMBA YENYE HATI NO. 36845 KIWANJA NA.370 KITALU "HHH" A" | KARANGA-MOSHI | 16/07/2021 NA KUENDELEA |
| 15 | NHJK8 EDEN AGRI- AQUA LIMITED | UBUNGO | WILLY WILLIAM BWEMELO | HATI NO. 136896, KIWANJA NO.747,KITALU "K" PUGU | PUGU MWAKANGA-ILALA | 16/07/2021 NA KUENDELEA |
| 16 | SASI SELEMANI KITUNDU | KIJITONYAMA | MWAJUMA SELEMANI KITUNDU | NYUMBA | GOBA-KUNGURU | 16/07/2021 NA KUENDELEA |
| 17 | RAHMA AHUMANI MKINDI | AGGREY | NYUMBA | MOHAMED A.SANGAWE | KISIWANI , KIGAMBONI | 23-07-2021 NA KUENDELEA |
| 18 | EVA JOHN MIHAYO | AGGREY | NYUMBA | DIDAS DONATUS NYAKIMWE | KINYAMWEZI | 21-07-2021 NA KUENDELEA |
| 19 | ALIST SALVATORY MUGASHE | AGGREY | NYUMBA | ALIST SALVATORY MUGASHE | MZINGA; KITUNDA | 30-07-2021 NA KUENDELEA |
| 20 | ELIZABETH LAMECK ELOSONGERA | AGGREY | NYUMBA | ELIZABETH LAMECKELISONGERA | MWEMBE BAMIA | 06-08-2021 NA KUENDELEA |
| 21 | VALENCE WILLIAM GALINOMA | ARUSHA | VALENCE WILLIAM GALINOMA | NYUMBA | MOSHONO KIJENGE | 16/07/2021 NA KUENDELEA |
| 22 | NOEL BETHIULE MBISE | ARUSHA | NOEL BETHIULE MBISE | NYUMBA | BAGATA ARUSHA DC | 16/07/22021 NA KUENDELEA |
| 23 | LOMAYANI EDWARD MOILO | ARUSHA | LOMAYANI EDWARD MOILO | NYUMBA | NGARAMTONI | 22/07/021 NAKUENDELEA |
| 24 | FELISTER JOHN KOSIANGA | ARUSHA | FELISTER JOHN KOSIANGA | NYUMBA | SEKEI | 20/07/2021 NA KUENDELEA |
| 25 | RICHARD GABRIEL PALLANGYO | ARUSHA | RICHARD GABRIEL PALLANGYO | NYUMBA | MAJI YA CHAI | 29 /07/2021 NA KUENDELEA |
| 26 | DISMAS MALLYA | ARUSHA | EMMANUEL NAFTAL NGUVILA | NYUMBA | SOKONI 1 | 27/07/2021 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishia ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754497396/ 0785335544/ 0714939933/ 0754376493/ 0768672367/ 0715363537
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

116339602

## Huduma za PBZ zachangia kutangaza Muungano

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya PBZ imesema kusambaa kwa huduma za kibenki zinazotolewa na benki hiyo katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar na Tanzania Bara kumechangia kwa kiwango kikubwa kutangaza umuhimu wa Muungano.

Kauli hiyo ilitolewa na Ofisa Mwandamizi Masuala ya Masoko na Uendelezaji wa Biashara wa benki hiyo, Mohamed Khakis Ismail, katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), maarufu Sabasaba.

Ismail alisema zipo faida nyingi ambazo zimeletwa na uwapo wa Muungano ikiwamo Benki ya PBZ ambayo imekuwa ikitoa huduma katika mikoa mbalimbali katika pande zote za Muungano na kuchagiza kuinua uchumi wa wananchi kutoka katika makundi tofauti.

"Tunafurahi na tunafarijika kwamba Muungano una faida kubwa na sisi kama PBZ tumetumia huduma zetu kuendelea kuutangaza hasa katika kuhakikisha wananchi wote wananufaika kupitia taasisi hii ya fedha kuinua uchumi wao na wa nchi kwa ujumla," alisema Ismail.

Alisema miongoni mwa huduma wanazotoa kwa ajili ya kusaidia makundi ya pande zote za Muungano ni pamoja na kutoa mikopo nafuu kwa vikundi vya vyama vya wakulima na masoko (AMCOS), ambavyo vinatambulika kisheria.

"Tumekuwa tukitoa mkopo kwa makundi ya wakulima wa korosho na karafuu na ni nafuu kwa sababu lengo lake ni kutaka viboreshe kilimo chao zaidi, kukuza uchumi wao na wa nchi kwa ujumla," alisema Ismail.

Alisema ili kupanua wigo wa utoaji wa huduma zao zaidi, wamejipanga kujitanua katika mikoa yote ya pande zote za Muungano.

Alisema kwa sasa wanatoa huduma Zanzibar na mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, na Mbeya.Ismail alitoa wito kwa vikundi mbalimbali kuchangamkia fursa katika kipindi hiki cha maonyesho ya Sabasaba kutembelea banda lao ili kupata elimu ya huduma mbalimbali za kifedha kwa ajili ya kuendeleza miradi yao.

"Maonyesho ya Sabasaba ni fursa kubwa sana, wanatakiwa kuichangamkia, wakija hapa PBZ watafahamu aina ya mikopo wanayotakiwa kuchukua na niwashauri waondoe ile dhana ya kuogopa kuchukua mikopo kwenye taasisi za kibenki bila kufika na kupata elimu sahihi, wasisikie yale wanayoambiwa, wakumbuke kwamba uchumi wao na wa nchi utakuwa bora kwa kufanya kazi kwa bidii kama Rais Samia Hassan Suluhu anavyotusisitiza kila mara," alisema Ismail.

# Madeni ushirika yakwamisha ununuzi pamba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWENYEKITI wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Emmanuel Charahani, aziomba taasisi za kifedha zilizokopesha vyama vya ushirika, kuviondolea ongezeko la riba ili kubaki na madeni halisi na kurejesha hatimiliki za mali walizoweka kama dhamana wakati wa ukopaji.

Charahani alisema hayo jana alipozungumza na vyombo vya habari ofisini huku akibainisha kwamba mpaka sasa chama chake kimeshanunua zaidi ya kilo 600,000 za pamba kutoka kwa wakulima wa Halmashauri za Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama.

Alisema viongozi wa taasisi hizo wakae na viongozi wa vyama vya ushirika kuangalia namna ya kurejesha madeni hayo na kuvikopesha upya ili vinunue pamba kuongeza ushindani na kampuni za ununuzi wa zao hilo na mkulima anufaike.

Ili kufanikisha hilo, alisema amewaomba Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuzishawishi benki hizo namna ya kuviondolea ongezeko la riba linalozidi kila mwaka ili kufufua ushirika na kumwinua mkulima.

Alisema mpaka sasa Chama cha Ushirika kinachonunua pamba ni KACU pekee huku vyama vingine vikishindwa kununua kutokana na kuwa na madeni makubwa na taasisi za kifedha na kushindwa kukopesheka na kununua zao hilo.

"Chama cha Ushirika SHIRECU (Shinyanga), Nyanza na KNCU (Kilimanjaro) hatimiliki za mali zao zimeshikiliwa na taasisi za fedha kwa kushindwa kulipa fedha walizokopa na kusababisha KACU kuendelea kununua zao hilo pekee. Vingekuwa vinanunua vingeongeza ushindani wa soko na mkulima kunufaika zaidi," alisema Charahani.

Pia alisema katika msimu huu bei halali ya ununuzi wa zao hilo ni Sh. 1,050 kwa kilo na kwamba walianza kununua kwa Sh. 1,100 baada ya kuona ushindani umekuwa mkubwa. Lakini kwa sasa wananunua kwa Sh. 1,300 na wanatarajia kununua kilo milioni 10 sawa na marobota 20,000 ya pamba.

Aidha, alisema msimu uliopita walinunua pamba kutoka mikoa ya Geita na Shinyanga kwa Sh. 920 na kupata zaidi ya kilo milioni 2.2 zenye thamani ya Sh. bilioni 3.1 na kurejesha malipo ya pili kwa kila kilo Sh.40 sawa na zaidi ya Sh. milioni 900.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo kutoka Msalala, Charles Mhoja, alisema kitendo cha KACU kununua zao hilo kimesababisha kuwapo kwa ushindani na kampuni zingine zinazofanya shughuli hiyo kutoka bei halali ya Sh. 1,050 hadi Sh. 1,300 kwa kilo.




Meneja wa Mawasiliano wa Tigo Tanzania, Woinde Shisael, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kampuni hiyo, kuwa mdhamini rasmi wa mawasiliano katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa kwa mwaka wa sita mfululizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ageukia mapambano dhidi ya corona

**Na Steven William,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, amewataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya corona kwa kutumia vifaa maalum, kunawa mikono kwa maji safi na sabuni pamoja na kufuata maelekezo ya wataalamu.

Moyo alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na waumini wa Kanisa la Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT) alipotembelea na kujitambulisha baada ya kuteuliwa kushika wadhifa huo hivi karibuni.

Alisema waumini wa kanisa hilo na wananchi wa Iringa hawana budi kuchukua tahadhari kujikinga na ugonjwa huo huku akiwaomba viongozi wa dini zote kuliombea taifa ili kutokomeza ugonjwa huo.

Kiongozi huyo alisema amefika wilayani Iringa kushirikiana na viongozi wa madhehebu ya dini zote huku akisema mlango wa ofisi yake uko wazi na kama kuna tatizo, mashehe, wachungaji, mapadri na maaskofu wafike ili wakae na kuyatatua.

Moyo alisema kazi iliyo mbele yake ni kufanya kazi kwa kushirikiana na watu wote bila kujali dini wal a itikadi za kisiasa ili kuwaletea wananchi maendeleo na kutatua kero zinazowakabili.

Naye Askofu wa Kanisa la EAGT Jimbo la Iringa, Ezekiel Mkenda, alishukuru mkuu huyo wa wilaya kumtembelea kanisani kwake na kuzungumza na waumini wa kanisa hilo kwa kuwa ni kiongozi wa kwanza katika nafasi hiyo kufanya hivyo.

Alisema kwa niaba ya kanisa, atahakikisha wanamuunga mkono katika kazi zake kwa kuwa ameonyesha heshima kubwa kwa muda mfupi baada ya kuwasili wilayani hapa.

Tangu awasili wilayani hapa baada ya kuteuliwa, Moyo amefanya ziara na kukutana na kufanya mazungumzo na maaskofu Joseph Mgomi wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Ruaha, Blaston Gavile wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa na Mchungaji Bora Benjamin wa Kanisa la Moravian Jimbo la Iringa.

HABARI KITAIFA

# Wahitimu elimu msingi, sekondari washauriwa

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

VIJANA hasa wa kike kutoka katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kagera ambao wamehitimu elimu ya darasa la saba na kidato cha nne na kuendelea na masomo, wameshauriwa kujifunza shughuli za ujasiriamali badala ya kukata tamaa ya maisha kutokana na kukosa ajira.

Wakizungumza katika maonyesho ya Sabasaba yanayoendelea katika Manispaa ya Bukoba, mmoja wa washiriki wa maonyesho hayo, Theresia Ntezibwa, alisema maonyesho hayo ni fursa kwa vijana kuyatumia kujifunza kazi za mikono ambazo zinaweza kuwaingizia kipato na kuacha utegemezi.

"Wapo kinamama wanakaa nyumbani hawataki kujishughulisha... enzi hizi zimepitwa na wakati, lakini pia kuna mabinti wana elimu ya vyuo na hawana ajira, hawapaswi kukaa tu na kuilaumu serikali kuwa hawana ajira badala yake wajifunze kazi za mikono wajiajiri," alisema Ntezibwa ambaye ni mwenyekiti wa kikundi cha ujasiriamali cha Makedonia.

John Kidua, mjasiriamali wa tiba za asili, aliwataka wakazi wa Mkoa wa Kagera wanaokwenda katika viwanja vya maonyesho kuchukua tahadhari kwa kuvaa barakoa na kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono wanapoingia, ili kuhakikisha wako salama kiafya.

Naye mkurugenzi wa shirika linaloandaa maonyesho hayo la Kaide, Philmon Kamazima, alisema wametekeleza maagizo ya serikali na kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa wa corona kwa kuweka vifaa vya kunawa mikono na kuhimiza wajasiriamali na wananchi wanaoingia eneo hilo kuvaa barakoa.

# Gharama umiliki ardhi zashushwa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI imepunguza gharama za umilikishaji wa ardhi kwa wananchi kwa kupunguza tozo kutoka asilimia 2.5 katika maeneo mapya ya ardhi na asilimia moja katika maeneo ya urasimishaji hadi asilimia 0.5.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Marry Makondo, alisema hayo mjini hapa, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Willium Lukuvi, wakati akifungua kongamano la kitaifa la masuala ya ardhi na maadhimisho miaka 20 ya utekelezaji wa Sheria za Ardhi nchini lililofanyika mkoani hapa.

Alisema serikali imeendelea kuwawezesha wananchi kumiliki ardhi kwa kupunguza gharama za umilikishaji kuanzia mwezi Julai, mwaka huu.

Makondo alisema serikali inatarajia kuongeza kasi ya umilikishaji ardhi na wananchi wengine wanaombwa kuhakikisha wanakuwa na ardhi iliyopangwa, kupimwa na kumilikishwa ili wawe na milki salama.

Vilevile, alisema Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imewataka wamiliki wa ardhi kutekeleza masharti ya umiliki wa ardhi ikiwamo kulipa kodi kwa wakati na malimbikizo ya madeni ili kuepuka kufutiwa hati zao ama kunyang'anywa.

Alisema yapo madhara ya kutolipwa kodi ambayo ni kutumiwa ilani ya kuonywa na baadaye kusudio la ubatilisho kwa kuwa ardhi yote ni mali ya umma na imekabidhiwa kwa Rais kwa niaba ya raia ni kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alisema sababu zinazochangia migogoro ya ardhi kuwa ni wananchi wa hali ya chini kushindwa kujitetea wanapopatwa na madhila ya kutaka kunyang'anywa vipande vyao vya ardhi.



Mshiriki wa mafunzo kuhusu uelewa wa bajeti yenye mlengo wa kijinsia, Kareny Masasy kutoka Shinyanga, akisisitiza jambo katika mafunzo hayo, yaliyoendeshwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na kushirikisha wanahabari na wanajamii, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wanawake wapewa mbinu kuboresha bidhaa

**Na Christina Mwakangale**

WITO umetolewa kwa wanawake wajasiriamali kuboresha bidhaa zao ili kuendana na ushindani na kulifikia soko lililoko barani Afrika lililo na takribani watu bilioni 1.2.

Katibu Mkuu wa Idara ya Usimamizi wa Soko Huru la Bara Afrika (AfCFTA), Wamkele Mene alitoa wito huo jijini Dar es Salaam, akizungumza na waandishi wa habari kwenye mkutano uliohusisha wajasiriamali, wazalishaji biashara za viwandani na taasisi.

Alisema kwa kuzingatia wanawake ndio waliojiajiri zaidi kwenye shughuli za ujasiriamali watahudhuria kongamano la kimataifa litakalofanyika mjini Accra, nchini Ghana, litakalohusisha nchi mbalimbali za Afrika ikiwamo Tanzania.

"Mkataba wa kuondoa vikwazo kibiashara kupitia AfCFTA umeridhiwa na nchi 39 kati ya zilizopo Afrika. Tanzania ikiridhia itafanya idadi kuwa 40. Matarajio ni nchi zote barani Afrika kuridhia ili soko la watu bilioni 1.2 liwe letu, kuuza na kuzalisha kuondokana na umaskini," alisema Mene.

Aliongeza kuwa biashara kati ya mataifa ya Afrika itakua kutoka asilimia 18 hadi kufikia 50 kupitia mpango wa pamoja wa kufungua fursa na kuondoa vikwazo kibiashara barani Afrika kupitia AfCFTA.

"Wanawake watainua uchumi wao kupitia mtandao wa pamoja na kiuchumi wakijumuka na biashara za muingiliano mipakani. Wakijengewa uwezo na kuongeza ubunifu katika biashara hayo yatawezekana ni sasa Afrika kuchukua hatua kusonga mbele," alisema Mene.

Alisema AfCFTA haujajikita katika kuweka makubalino ya kiuchumi kwa nchi zilizoridhia bali umelenga kuinua wananchi milioni 100 wa nchi zilizoridhia na kupunguza umaskini ifikikapo 2030, kutokana kufanya biashara kutambuliwa rasmi na kisheria.

Mkurugenzi Idara ya Biashara,Uwekezaji na Sekta za Uzalishaji, kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Benard Haule, alisema serikali ipo kwenye hatua za mwisho kuandaa sheria kupitia bunge, Septemba mwaka huu, ambayo itaifanya Tanzania kuanza kutekeleza mpango wa AFCTA ambao utaridhiwa.

Mkurgenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Francis Nanai, alisema mpango huo ni fursa kwa sekta hiyo, kwa kuonyesha biashara zao zikiwa na ubora zilizobuniwa ili kukabiliana na ushindani sokoni.

"AFCFTA utaleta utatuzi kwa matatizo yaliyopo katika sekta hii, ikiwamo viwanda na kusaidia kulinda biashara zetu katika soko la ukanda ambalo limeajiri watu wetu wengi," alisema Nanai.

# Wakaguzi wenye ithibati ya umahiri wapewa fursa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAGUZI wenye ithibati ya umahiri nchini wametakiwa kutumika kipindi, ambacho Tanzania inatekeleza miradi mingi mikubwa ya ujenzi na maboresho ya miundombinu, ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza baada ya ujenzi kukamilika.

Ushauri huo ulitolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Lazaro Mwambole, wakati akizungumza kwa niaba ya mkurugenzi mkuu wa shirika hilo, Dk. Yusuf Ngenya kwenye Maadhimisho ya Siku ya Ithibati ambayo yaliadhimishwa na shirika hilo jijini Dar es Salaam.

Alitoa mifano wa miradi hiyo inayohitaji wakaguzi wenye ithibati ya umahiri ni ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ambayo inatumia umeme, ujenzi wa barabara za juu, ujenzi wa bomba la mafuta, ujenzi wa barabara za mabasi yaendayo haraka na mengine.

"Kuna mahitaji mbalimbali katika ujenzi wa miundombinu na majengo ambayo ni malighafi, bidhaa za ujenzi na wakaguzi wenye ithibati ya umahiri ili kuepuka madhara ambayo yanaweza kujitokeza baada ya ujenzi kukamilika," alisema Mwombole.

Kutokana na umuhimu huo, alitoa wito kwa wadau wote kwenye mnyororo wa ugavi kutumia maabara zilizo na mifumo ya kimataifa ili kupata vipimo sahihi na vinavyokubalika kimataifa.

Alitolea mfano nchi zilizoendelea, akisema kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa malengo ya ajenda 2030 ya Maendeleo Endelevu hufanikiwa kwa kutumia viwango pamoja na huduma zinazotolewa na taasisi zenye ithibati ya umahiri kwenye upimaji, ugezi, ukaguzi na uthibitishaji ubora.

"Katika nchi hizo ithibiti ya umahiri hutumika kama kigezo muhimu kuondoa vikwazo vya kibiashara na kukuza uchumi wa nchi, kukuza pato la taifa na kupunguza umaskini," alisema Mwombole.

Alitoa wito kwa wadau mbalimbali kujiuliza ni kwa jinsi wanaweza kutumia ithibati ya umahiri kutekeleza malengo ya ajenda 2030 ya maendeleo endelevu.

## Utendaji bandarini waiibua sekta binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

TAKRIBANI miezi mitatu tangu Rais Samia Suluhu Hassan afanye mabadiliko ya uongozi katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imeelezwa kuwa ufanisi umeanza kuonekana kwa kuwa huduma zimeboreshwa na kufanya sekta binafsi kuridhishwa na utendaji kazi.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Angelina Ngalula, amepongeza utendaji kazi wa TPA na kusema matarajio ya wadau na watumiaji wa bandari ni kuona huduma bora na ufanisi.

"Tunapongeza hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na TPA kuhakikisha mizigo bandarini inaondolewa kwa wakati bila ya ucheleweshaji wowote," alisema Ngalula.

Alisema matokeo chanya ya muda mfupi yametokana pia na kamati iliyoundwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa kushirikisha wadau na mamlaka kuondoa changamoto mbalimbali zilizokuwa bandarini.

"Changamoto kubwa ilikuwa ni uratibu, hivyo kuundwa kwa kamtati ya uboreshaji wa bandari ambayo inaongozwa na Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi imeleta mafanikio makubwa kwa muda mfupi," alisema Ngalula.

## Serikali kujikita utafiti wa maziwa

**Na Zuwena Shame**

Serikali imesema imedhamiria kushirikiana na sekta binafsi ili kufanya utafiti mbalimbali utakazosaidia sekta ya maziwa nchini kuwa na tija na kuongeza pato la mfugaji na taifa kwa ujumla.

Aidha utafiti huo utawezesha zao la maziwa kwa kusaidia a kuongeza mnyororo wa thamani kwa kutengeneza bidhaa za zitokanazo na maziwa.

Hayo yalisema jijini Dar es salaam juzi na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (anayeshughulikia sekta ya mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, wakati wa ghafla ya kukabidhi vyeti kwa washindi wa shindano la wauza pembejeo za kilimo lilliloendeshwa na tassisi ya AgResults katika mikoa ya Pwani, Tanga, Dar es Salaam na Morogoro.

Ole Gabriel alisema kwa sasa Tanzania inashika nafasi ya pili kwa uzalishaji wa maziwa Afrika , hivyo ni muda sahihi kuweka nguvu katika sekta hiyo kwa kufanya utafiti utakaosaidia mchakato mzima wa mnyororo wa thamani.

Alisema kuwa katika nchi mbalimbali sekta ya maziwa imekuwa inchangia pato la taifa, hivyo hata Tanzania inaweza kuiga mafanikio hayo, kwa kukaribisha wawekezaji na kuzalisha bidhaa nyingi za maziwa.

Aliongzea kuwa takwimu zinaonyesha sekta ya maziwa inaongezeka kila mwaka na kuchangia pato la taifa kwa asilimia 7.4.

Mratibu wa mradi wa AgResults , Neema Mrema, alisema wafugaji wengi wa ng'ombe wa maziwa nchini wanakabiliwa na vikwazo hivyo kusababisha vya uzalishaji duni wa maziwa, hilo linasababishwa na kutopatikana pembejeo bora na huduma za ushauri na ugani.




Maofisa wa Wakala wa Usajili na Ufilisi (BRELA) wakitoa maelezo kwa wateja waliotembelea banda lao, katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa katika viwanja vya Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wenye ulemavu wa kusikia wamwomba Rais Samia

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MWENYEKITI wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Mkoa wa Pwani, Adam Shaban, amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwakumbuka wenye uziwi kwenye teuzi zinazoendelea ili wapate mtu wa kuwasemea kero zao.

Wameomba kuangaliwa katika uteuzi ili nao wawe na wawakilishi kwenye vyombo vya uamuzi kama ilivyo lwa makundi mengine ya watu wenye ulemavu.

Adamu alifikisha ombi hilo kwa Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, ambaye alikwenda kufungua semina ya elimu ya afya kwa viziwi iliyofanyika juzi kwa ufadhili wa Shirika la Abil Foundation.

Alisema kundi hilo lina wasomi wengi ambao wanaweza kushika nafasi za uongozi na kumsaidia Rais katika masuala mbalimbali, lakini halijakumbukwa na si katika nafasi za uteuzi pekee bali hata katika wabunge.

"Tumefurahi kukutana na wewe kwenye semina yetu kikubwa tunachoomba umfikishie Rais ombi letu hili, na sisi tunapenda kuona mmoja wetu akituwakilisha ngazi za juu, atusemee kero zetu zitafutiwe ufumbuzi wa haraka," alisema.

Aidha, aliiomba serikali kusaidia suala la wakalimani kwenye vituo vya afya ili kurahisisha kundi hilo kupata huduma.

Akifungua semina hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, alisema amepokea maombi hayo, huku akiahidi kuendeleza ushirikiano kati ya serikali na kundi hilo.

Sara aliwataka wafadhili kuhamasisha uundaji wa vikundi kwa watu wenye ulemavu ili wanufaike na mikopo kutoka halmashauri, ambayo itawasaidia kujiinua kiuchumi.

Meneja wa Mradi, Anna Gugu, alisema mradi huo wa elimu ya afya kwa vijana na wanawake wasiosikia Mkoa wa Pwani utatekelezwa katika halmashauri nne ambazo ni Kibaha Mjini, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Chalinze na Bagamoyo.

## Korea yatoa mamilioni kufadhili mafunzo vijana

**Na Hellen Mwango**

MAMLAKA ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA) imeingia makubaliano na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Korea (KOICA) kwa ajili ya mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana 4,000 katika mikoa ya Dodoma, Lindi na Manyara.

Kadhalika vijana hao watanufaika na mafunzo na kuwajenga kuwa na utayari wa kuajiriwa au kujiajiri kupitia mradi wa ajira na ujuzi kwa maendeleo ya Tanzania.

Makubaliano ya mradi huo yalitiwa saini Dar es Salaam kati ya Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Dk. Pancras Bujulu na Mkurugenzi Mkazi wa KOICA nchini, Kyucheol Eo.

Eo alisema serikali yake imetenga Dola za Marekani 5,300,000 kwa ajili ya mradi huo utakaotekelezwa kwa miaka mitatu kuanzia mwaka huu.

Pia VETA itashirikiana kwa karibu na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ) katika utekelezaji wa mradi huo ili kuhakikisha vijana wa Tanzania wananufaika na ukuaji wa uchumi katika sekta zinazotegemea ujuzi wa ufundi stadi.

Naye Dk. Bujulu aliishukuru Serikali ya Korea kwa ufadhili huo na kusema mradi huo umejikita katika kutoa mafunzo ya muda mfupi kwenye fani za uchomeleaji, ufundi bomba wa viwandani na mekatroniki.

Alisema mradi huo pamoja na mambo mengine, utawapatia vijana hao mafunzo ya ujasiriamali na kutoa fedha kama mtaji ili kuwawezesha wahitimu kuanzisha miradi yao na kuwawezesha kujiajiri. Mitaji hiyo itatolewa kwa timu za wanafunzi zitakazoshinda kupitia uwasilishaji wa miradi bora itakayopatikana kupitia shindano maalum la ujasiriamali litakalofanyika kila mwaka.

# Msimamo wa uongozi CPC, chaguo la kihistoria, watu wa China

## Na Xu Chen, Kaimu Balozi wa Jamhuri ya Watu wa China China


JANA watu kutoka makundi yote ya kijamii ndani ya China, kwa taadhima waliadhimisha mwaka wa 100 tangu kuanzishwa kwa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC).

Kwa kipindi cha miaka 100 iliyopita, Chama cha CPC kimekua kutoka mwanzo wake wa chama kidogo chenye wastani wa wanachama 50 tu, hadi kufikia hadhi ya chama kikubwa zaidi duniani, kikiwa na wanachama takriban milioni 95.

Katika miaka 100 iliyopita, kikiwa na dhamira yake ya asili ya kuwatafuta furaha watu wa China inayoendana na lengo la kuliinua upya taifa la China, CPC imewaongoza watu wa China katika jitihada zao za kuwasaidia, kuwajengea hamasa na kustawisha nchi hatua kwa hatua, na hatimaye kuleta mabadiliko kamili ya taifa kutoka kwenye umaskini, udhaifu, kuonewa na kudharauliwa na majeshi ya kigeni, hadi kuhamia taifa lenye hadhi na ushawishi kamili duniani kote.

CPC imetengeneza muujiza katika historia ya taifa la China na historia ya maendeleo ya kijamii duniani, hivyo kutoa michango ya kihistoria kwa nchi, watu wake na dunia.

Chama cha Kikomunisti cha China kimepigana kwa dhamira ya kujizatiti kwa uimarishaji wa taifa na kuifanya China isimame imara katika Ukanda wa Mashariki.



Xi Jinjing, Katibu Mkuu wa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC), Rais wa China na Mwenyekiti wa Tume Kuu ya Jeshi, akitoa hotuba muhimu katika Maadhimisho ya Miaka 100 ya CPC jijini Beijing jana. PICHA: **XINHUA/JU PENG**

Wakati CPC inazaliwa mwaka 1921, China ilikuwa katika hadhi ya nusu-koloni na nusu umwinyi, taifa likiwa katika hatari ya kutokomea.

Kupitia miaka 28 ya mapambano magumu, CPC iliwaongoza watu wa China kukamilisha mapinduzi mapya ya kidemokrasia na kuunda Jamhuri ya Watu wa China, ikaingiza taifa jipya la China katika zama mpya.

Baada ya kuundwa kwa China Mpya, CPC iliwaongoza watu wa China kukamilisha mapinduzi ya kijamaa na na kuuanzisha ujamaa wa msingi.

Haya ndiyo mabadiliko makubwa zaidi na mageuzi ya kimsingi katika katika historia ya China, ambayo yaliweka msingi muhimu



Tukio la kupandisha bendera mbele ya mkusanyiko wa watu waliofika kwenye Maadhimisho ya Miaka 100 ya Chama cha Kikomunisti cha China (CPC), katika eneo la Tian'anmen Square jijini Beijing, China jana. PICHA: **XINHUA/PANG XINGLEI**

wa kisiasa na mfumo mama wa mabadiliko na maendeleo ya China hadi sasa.

Katika miongo minne iliyopita, CPC imewahamasisha watu wa China kujenga mapinduzi mapya matukufu ya urekebishaji na kufungua nchi, kuanza kufuata mwelekeo wa Ujamaa wenye vianzio vya Kichina. Watu wa China walipiga hatua na kuanza kuibukia kwenye hadhi ya kitajiri.

Tangu Mkutano Mkuu wa 18 wa CPC mwaka 2012, chini ya uongozi wa Kamati Kuu na Katibu Mkuu Xi Jinping kama mzizi wao, chama na taifa kwa ujumla wamefanya mengine zaidi na kufikia mafanikio ya kihistoria.

Ujamaa wenye misingi ya kichina ilimeingia kwenye zama mpya na watu wa China wanasonga mbele kuwa imara na shupavu zaidi.

Historia imedhihirisha kuwa bila ya kuwapo uongozi wa CPC, kusingekuwapo China Mpya ya leo na nchi isingeweza kupata mafanikio yote na hadhi ya kimataifa inayofurahia sasa.

CPC imebadili kwa msingi yake muskatbali wa baadaye na mwelekeo wa taifa na watu wake, hata ikaibua miujiza miwili. Wa kwanza, ni kasi kubwa ukuaji uchumi. Ikianzia na ngazi ya chini zaidi, China ikakamilisha ndani ya miongo miochache kuinmgia katika ulimwengui viwanda, ambaonchi zilizoendelea zilichukua karne kadha kuufikia na imeobuka kufikia kigogo wa pil wa uchumi mkubwa zaidi duniani. Muujiza wa pili, ni uthabiti wa kijamii uliodumu kwa kipindi kirefu sana. Jamii ya Kichina imebaki thabiti na yenye utangamano, watu wake wanaishi na kufanya kazi kwa amani na wenye kuridhika. China ni moja ya nchi zenye usalama zaidi inayotambulika mbele ya jumuiya ya kimataifa.

Leo, China iko karibu zaidi, inajiamini zaidi na inajiweza kuliko wakati wowote ule, ikiweka malengo yake ya kuliinua taifa upya zaidi yanatimia kuwa hali halisi.

Shukurani za kipekee zinawaendea wana -CPC na juhudi za pasipo kuchoka, katika kuwaletea ustawi watu wao, watu wa China sasa wamekuwa ndiyo wakubwa wa nchi yao, jamii na hatima yao wenyewe. Tangu izaliwe, CPC imekuwa ikiwachukulia kuwatumikia watu kwa moyo mmoja ndiyo dhamira yake msingi na ikijielekeza katika tumaini la watu kuishi maisha bora zaidi.


Kwa kutumia juhudi za pamoja pasipo kukata tamaa, CPC na watu wa China wamekuwa wakipigana kufanikiwa kupata mengi maishani, wawe na furaha na wenye kujiamini.

Chini ya uongozi wa CPC, watu wa China wanashiriki kikamilifu katika utawala wa nchi yao na kunufaika na haki na uhuru, unaolindwa na taasisi kama Chombo cha Uamuzi (Bunge)

na inawafikisha katika kina kirefu cha matumizi ya utawala wa sheria kwao.

Hali ya maisha ya watu wa China imeboreka kwa kiwango kikubwa, wastani pato mtu mmmoja mmoja inazidi Dola za Marekani 10,000 ndai ya kipindi cha miaka miwili mfululizo na kiwango cha fedha kwa mtu wa kawaida kuwa mara 600 ikilinganishwa na mwaka1949 wakati China Mpya ilipoundwa.

China inaendesha mfumo mkubwa zaidi wa hifadhi ya jamii duniani, ambako kuna



**Rais Xi Jinping wa China, alipozuru Afrika kwa mara ya kwanza, na kuichagua Tanzania kama kituo cha kwanza Machi 24, 2013**

uhakika wa bima ya afya ya msingi inayojumuisha jumla watu bilioni 1.36 na bima ya pensheni nayo imefikia karibu watu bilioni moja.

Tangu kuanza kwa utekelezaji wa mageuzi na kufungua nchi, wakazi milioni 770 wa vijijini wameshaondolewa kutoka hali ya umaskini waliokuwa nayo, ambao ni zaidi ya asilimia 70 ya hatua ya uondoaji umaskini kwa watu wote duniani kwa wakati huo.

China ilifikia lengo la kuondoa umaskini lililowekwa na Ajenda 2030 ya Umoja wa Mataifa kwa Maendeleo Endelevu miaka 10 kabla ya muda uliopangwa.

Katika hatua ya kwanza ta mlipuko wa janga la corona, CPC iliwweka mbele watu wake na maisha yao na ikalinda afya na usalama wao kwa nguvu na gharama zote. Ndiyo maana China imefikia hatua kubwa ya kimkakati katika kupambana na virusi hivyo.

Kwa kuwa CPC imetanguliza maslahi ya watu wake wakati wote, hili limeifaye iaminiwe, ikubalike na kuungwa mkono na watu wa China. Kura ya maoni iliyofanywa na tasisi ya utafiti ya Edelman mwaka 2020, ilibaini asilimia 95 ya watu wa China wana imani na serikali yao, hali inayoiweka China juu zaidi ya nchi zote zilizofanyiwa utafiti kama huo.

Chama cha Kikomunisti cha China kinasisitiza katika jitihada za maendeleo ya binadamu na kuleta mabadiliko ya msingi katika maendeleo ya dunia.

Katika miaka 100 iliyopita, imejitoa kuweka mchango mopya na mkiubwa zaidi kwa binadamu. CPC mara zote imekuwa mjenzi wa amani dunia, mchangiaji maendeleo kote na mlinzi wa misimamio na itifaki za kimataifa. CPC imewaongoza watu wa China kushinda Vita vya Kujilinda dhidi ya Uvamizi wa Japan, ikatoa mchango mkubwa katika ushindi wa Mfungamano wa Dunia dhidi ya Ufashisti.

Baada ya kuundwa kwa Jamhuri ya Watu wa China, CPC ilifanya kila ilichoweza kuunga mkono mataifa yanayokandamizwa duniani, katika jitihada zao za ukombozi kitaifa, uhuru na maendeleo ya kiuchumi, inayodhihirishwa na kujengwa kwa reli ya TAZARA.

China ilianzisha Kanuni Tano za Ushirikiano kwa Amani na imekuwa ikitetea maendeleo ya amani duniani. China inaunga mkono kwa vitendo na inashiriki katika kazi za Umoja wa Mataifa katika nyanja tofauti na imeunda nyenzo nyingi za ushirikiano kimataifa, kama vile Jukwa la Ushirikiano wa China na Afrika, Jukwaa la China na Latini Amerika na ushirikiano na nchi za Caribbean, Jukwaa la Ushirikiano wa China na Nchi za Kiarabu, n.k.

Maono na matendo ya chama cha CPC katika kustawisha amani ya dunia, yamefanikiwa sana kutambulika kimataifa.

Ikikabiliana na changamoto kuu zinazoikabili dunia, Katibu Mkuu Xi Jinping amebuni wazo la kuijenga jumuiya yenye mtazamo wa pamoja wa baadaye kuhusu utu wao.

China inapendekeza 'Wazo la Mkanda na Barabara' unaoweka mahitaji ya watu na nafasi kwa maendeleo ya dunia, hasa kwa nchi zinazoendelea.

Tangu mfumuko wa janga la corona, China imejitoa kuinua ushirkiano kimataifa kupambana na wimbi la maambukizi, imechangia uzoefu katika kuzuia maambikizi ya Covid - 19 na nchi nyingine na imetoa misaada ya vifaa tiba vya kupambana na maradhi kwa zaidi ya nchi 150.

Pia, imetoa dozi milioni 450 za chanjo kwa nchi tofauti duniani kote. China haichoki katika ujenzi wa jumuiya ya afya njema kwa binadamu wote.

CPC imeendelea kubadilishana na kushirikiana na vyama zaidi ya 400 vya kisiasa duniani kote. Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni rafiki wa karibu wa CPC. Kwa miongo kadhaa vyama hivyo viwili vimeshirikiana furaha na majonzi, inayotoa mchango tangulizi katika kujenga uhusiano wa pamoja kati ya nchi hizi mbili.

Mwaka 2018, majadiliano ya ngazi ya juu kati ya CPC na vyama vya Afrika, Mkutano wa Ngazi za Juu wa CPC katika Mazungumzo na Vyama vya Siasa Duniani, ukifuatilia mada maalum kuhusu Afrika, ulifanyika kwa mafanikio makubwa nchini Tanzania.

Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Tanzania mwaka 2020, CPC na serikali ya China vilichukua msimamo usio na shaka kuunga mkono juhudi za Tanzania kufanya uchaguzi huo bila kuingiliwa na kwa utulivu.

Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM, alimwandika barua Katibu Mkuu Xi Jinping, akiipongeza CPC kwa maadhimsho ya miaka 100. Yote haya ni ishara ya urafiki wa 'Marafiki na Ndugu' kati ya CPC na CCM.

Ikiwa imesimama katika mwanzo mpya wa kihistoria kwa kuinuliwa zaidi kwa taifa la China, CPC inaonyesha nguvu mpya na cheche za uhai katika kuwaongoza watu wa China katika safari yao ya kujenga nchi ya kisasa ya kijamaa katika nyanja zilizotimia.

CPC iko tayari kushikana mkono kwa mkono na CCM na vyama vyote na watu duniani kote, kubasdilishana mawazo kuhusu fursa za maendeleo, kufanya kazi pamoja kwa ajili ya maendeleo na kutoa michango zaidi ya ujenzi wa jumuiya yenye hatima ya pamoja kwa binadamu wote.



**Xi Jinping akiwatembelea watu watu wanaoishi katika lindi la umasikini kwenye Kaunti ya Fuping, Mkoa wa Hebei. Kilicho muhimu juu ya kukamilisha jamii yenye ustawi ni heshima kwa mambo yote.**



**Kiongozi wa China, Deng Xiaoping, alipokutana na Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, jijini Beijing Novemba 23, 1989.**

# Barua ya pongezi kutoka kwa Mh. Mizengo P. Pinda, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Urafiki kati ya Watu wa China na Tanzania katika Maadhimisho ya Miaka 100 ya kuundwa kwa chama CPC (1921-2021)



CHAMA cha siasa hutoa tamko la pamoja kuhusu matarajio na dhamira ya makundi tofauti ndani ya jamii.

Vyama tawala huwa vinahalalishwa na sehemu kubwa ya watu, kwa kuwahakikishia mahitaji yao na kutetea ustawi wa jamii wakati wanayalinda maslahi ya taifa.

Inakuwa imeaminiwa na watu na kuweka rekodi ya chama kufikisha malengo yao, pia kuendelea kushika uhalali mkubwa wa kusimamia masuala ya umma kwa muda mrefu.

Wakati sasa kinaadhimisha miaka 100 tangu kuundwa, Chama cha Kikomunisti cha China, kimekuwa mfano wa dira kisiasa inavyoendeshwa kwa kushikilia mwanga wa mwelekeo wa maslahi ya maendeleo ya nchi, wakati huo huo kinadumu mioyoni mwa watu wake wakati wote.

CPC imeendelea kushikilia imani hiyo ya watu wa China. Kwa kiwango chochote kile, hiki kinavutia, pia ni mafanikio yanayotakiwa.

Kwa maoni yangu, vyama vya siasa duniani bila ya kujali muundo au mrengo wake, vinaweza kujifunza kutoka mafaniko hayo ya CPC.

Vyama vya siasa vina mchango mkubwa katika kuliunganisha taifa kuhakikisha mshikamano ambao CPC imeufikia kwa kiwango kikubwa.

Muundo wa uongozi wa CPC na mafanikio yake yaliyopitia vizazi kadhaaa vya viongozi, imedumisha malengo na dhamira ya msingi kutoka kwa viongozi waasisi, ikiweza kuidumisha kwa kupitia kipindi cha maji kutuama na yaliyotibuka, kuepuka wasipotoke kutoka nje ya ajenda yao kuu ya muda mrefu.

Chama cha CPC kimeendelea kuweka kando machafu katika siasa zake, ikiwamo rushwa, utovu wa nidhamu kutoka kwa makada wake wa ngazi zote, upendeleo n.k.

Badala yake kwa utashi mkubwa imedumisha kufuata utawala wa sheria ili kutetea uhuru wake na msimamo huru unaojitegemea, wakati huo huo inaendeleza kujinufaisha na rasilimali zake kwa faida ya watu wote wa China.

Ndani ya hatua zake hizo, imeendelea kudumisha urafiki na ushirikiano wa kihistoria na marafiku wa karibu, pia vyama vya siasa vinavyofanana yao kimtazamo duniani.

Kwa miaka yote, CPC na viongozi wake imemudu kuendana na mabadiliko ya kimazingira yanayojiri kutoka ndani na nje ya nchi.

Ndani ya nchi, fikra kuu kuanzia kwa wanachama wake katika mtazamo wa kiuchumi na sura pana ya idadi ya watu, imebadilika kwa kiasi kikubwa.

Katika mtazamo wa nje, matarajio ya wanachama hao wamejidhihirisha kwamba yako juu kwa CPC na taifa lao la China lina nafasi kubwa katika kuchangia mambo ya dunia.

Eneo lingine linaangukia katika uaminifu kwa uwezo wa chama CPC, kwamba kina uwezo wa kuongoza mwelekeo wa mafanikio kijami na kiuchumi kwa kizazi chao cha sasa na kijacho.



**Wazee katika Kaunti ya Zouping, Mkoa wa Shandong, wakipokea pensheni zao. China inaendelea kuimarisha sera yake ya mageuzi ya usalama na matunzo ya jamii, kuwahakikishia mahitaji ya kimsingi. Hatua kwa hatua imeanzisha mfumo mkubwa zaidi wa usalama wa kijamii duniani unaowajumuisha wakazi wa mijini na vijijini.**

CPC imethibitishia dunia kwamba nchi inaweza kuchagua na kudumisha njia yake ya maendeleo inayoifaa hkufikia maendeleo ya kiuchumi.

Sisi tulioko katika nchi zinazoendelea, tunaendelea kujifunza kwa umakini namna CPC ilivyoweza kuwainua mamilioni ya watu wa China, kutoka kwenye umaskini ndani ya kipindi kifupi.

Jitihada za Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambazo zinaendelea kujenga mazingira rafiki kwa ajili ya watu wa China kufikia mafaniki makubwa zaidi kiuchumi, kijamii na kiteknolojia, zinapaswa kupongezwa.

Ni vigumu katika hilo kutoutambua mchango wa CPC katika historia ya mafanikio ya China.

CPC inajenga mfano bora wa chama cha siasa kilichoweka dhamira na kubaki kuwa usafiri sahihi wa utawala wa umma kwa nchi zinazoendelea.

Kwa hiyo, nchi nyingi zinazoendelea za Kiafrika na kama zilivyo zingine nyingi duniani, hatuna budi kuendeleza uhusiano katika ya chama kimoja na kingine na wakongwe CPC.

Uhusiano huu unabaki kuwa msingi mkuu katika kuendeleza uhusiano wan chi moja na nyingine.

Pia, uhusiano kati ya Tanzania na China Tanzania unaweza kutafsiriwa kwa kina kwa namna yoyote na kipindi kirefu.

Hakuna anayeweza kupinga mavuno muhimu kutoka uhusiano kati ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na CPC katika kubofresha uhusiano kwa nchi hizo mbili ulipoanza mwaka 1978, walihakikisha kila upande unaendelea unaukuza na kuuimarisha sambamba na heshima ya pande zote.

Licha ya kuwa miongoni mwa vyama vikonge barani Afrika, CCM bado inaendelea kujifunza mengi muhimu kutoka kwa ndugu zao CPC, ambayo imeiwezesha CCM kudumu kuwa mvuto katika mioyo ya Watanzania.

Jambo hilo limeifanya CCM kuwa mzizi wa chama kinachopendwa tangu uhuru wa nchi mwaka 1961, licha ya kuwapo mabadiliko ya kisiasa.

Kilichofikiwa sasa, Tanzania imeingia kwenye hadhi ya uchumi wa kati, miaka mitano kabla ya kipindi kilichotarajiwa.

CCM bado ina safari ngumu kuhakikisha inapata mafanikio zaidi ya kiuchumi na kudumisha iliyoyafikia. Hiyo ndiyo nguzo ya Ilani ya chama tawala .

Inavutia kuona CCM inachukulia kwa umakini wajibu wake wa chama tawala na kuiendesha serikali ya Watazania kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Sisi Watanzania bado tunaendeleza mtazamo wa kushirikiana na vyama rafiki kimataifa, ikiwamo CPC ituunge mkono katika hilo tunalolifanya.

Tuko makini kutafsiri katika matendo uhusiano wetu wa kisiasa, kwa kuongeza fursa za kiuchumi, hususan kupanua masoko ya bidhaa zetu za shambani na maliasili, vivyo hivyo kuvutia mitaji mingi ya uwekezaji nchini, ambayo tunaamini marafiki wetu wa China wanaweza kutusaidia.

Kwa fursa hii, nina furaha kuitakia CPC heri ya maadhimisho. Ninawatakia viongozi na wanachama miaka mingine 100 ya mafanikio kama haya.

Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Chama cha Uhusiano wa China na Tanzania, Dk. Salim Ahmed Salim, na kwa niaba yangu binafsi kama Mwenyekiti Mwenza na Mjumbe Mwandamizi wa Kamati ya Ushauri ya China Institute for South-South Cooperation in Agriculture (CISSCA) na mjumbe wa Silk Road Think Tank Association (SRTA), ninapenda kuwatakia maadhimisho mema yaliyoanza jana tarehe Mosi, Julai 2021.

**Mizengo Peter Pinda**
**Waziri Mkuu mstafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**
**Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Urafiki baina ya China na Tanzania;**
**Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM);**
**Juni 29, 2021**



**Wataalamu kutoka China, Tanzania na Zambia wakishiriki ujenzi wa reli. Mnamo Julai 1976, Reli ya Tanzania na Zambia, iliyojengwa kwa pamoja, ilifunguliwa rasmi. Reli hiyo yenye urefu wa kilometa 1,860.5 ilikuwa moja ya miradi mikubwa zaidi ya misaada ya kigeni ya China na imekuwa ukumbusho wa urafiki kati ya China na Afrika.**

# Afrika Kusini mwa Sahara inajifunza nini kutoka mageuzi viwanda ya CPC?



**Na Dk. Darius Mukiza**

CHAMA cha Kikomunisti cha China (CPC) kinasherehekea karne moja ya kuanzishwa kwake. Katika miaka 100 iliyopita, CPC imetoa mchango mkubwa kuifkisha China kuwa ya viwanda.

Siyo tu imeweka msingi wa kukua kwa viwanda kwa kuunda Jamhuri ya Watu wa China (PRC), bali imefanya juhudi za kina kutafuta njia sahihi ya kuyafikia mafanikio hayo.

Wakati CPC inaanzishwa mwaka 1921, China ilikiwa jamii yab nusu koloni na nusu umwinyi na hakukuwapo hadhi ya kitaifa.

Sehemu kubwa ya watu wa China walikabiliwa na umaskini, misuguano ya kijamii na ukandamizaji kutoka nje. Ilikuwa iliyowaongoza watu wa China kuja juu na kupambana, kujenga umoja wa kiharakati katika vita dhidi ya uvamizi wa Japan, na kuupindua utawala wa kuzuia mabadiliko wa Kuomingtang.

Matokeo yake, ndiyo kukaundwa Janhuri ya Watu wa China mwaka 1949 na watu wa China wakakombolewa kutoka unyanyasaji wa nguvu za mamwinyi, mabeberu na mabwanyeye uchwara wa dola iliyokuwapo wakati huo katika harakati iliyoitwa 'Milima Mitatu.'

Tangu hapo, China ikaingia katika kipindi kipya cha kihistoria ikijenga taifa imara la kijamaa lenye mafanikio makubwa..

Kutokana na kukosa uzoefu wa ujenzi wa nchi ya kijamaa, China ilipitia magumu. Kwa kujenga mfumo wa Uzalishaji wa Pamoja kueneza wimbi la Mapinduzi ya Kitamaduni, CPC ilipata vikwazo katika maendeleo yake ya kiuchumi na uthabiti wa kijamii.

Hadi kufikia mwisho wa miaka ya 1970, uchumi wa China ulikkaribia kuanguka na sehemu kubwa ya watu wake walikuwa bado wanaishi katika lindi la umasikini.

Ishara ya pongezi za kipekee kwa uongozi wa Deng Xiaoping, kiongozi mkuu wa China wakati huo, CPC ilianzisha mageuzi na yaliyoufungua uchumi ulioiwezesha nchi kufikia mwelekeo chanya wa uchumi wa viwanda.

Hadi mwisho mwa miaka ya 1970, wastani wa pato la taifa kwa kila mtu wa China, lilikuwa chini ya robo kulinganisha na mkazi wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Lakini, baada ya miaka 40 ya hatua ya maendeleo, wastani huo wa mtu wa China sasa ni mara nne ya ya yule apatikanaye Kusini ya Sahara.

Wakati ambaye awali alikuwa juu kiuchumi hadi sasa anaendelea kupambana na hali aliyokuwa nayo miaka 40 iliyopita, ikiwa azma ya kubadikli hali ngumu vijijini na kuondoa lindi la umaskini, China imeshafikia mapinduizi ya viwanda katika upeo wa juu na kuufuta kabisa umaskini wa kutisha kwenye ardhi yake.

Nini kilileta tofauti hii kubwa ya matokeo ya uchumi kati ya China na Kusini mwa Afrika?

Kwa maoni yangu, CPC ilifanya vitu vitatu kwa usahihi, yaliyoiwezesha China kuwa ya viwanda. Cha kwanza, ni kudhibiti ongezeko la watu.

Wakati CPC ilipoanzisha sera ya mtoto mmoja, ili kuzuia ongezeko la watu mwaka 1980, idadi ya watu wakati huo ilishafikia milioni 987, huku kukiwapo kasi ya ongezeko la haraka (wastani wa asilimia 1.4 kila mwaka).

Viongozi wa CPC waliamini kwamba ongezeko hilo lisingedhibitiwa, basi idadi ya watu wa China hadi mwaka 2000 ingefika bilioni 1.3 na hadi kufikia 2010, idadi hiyo ingefika watu bilioni 1.5.

Athari yakera anaitaja kwamba ingeleta China magumu katika katika kuiunda China ya Viwanda, kwani sehemu kubwa ya utajiri wa nchi ambao ungeongezeka, ungetumika kulea watoto na kasi ya taifa kulimbikiza ziada ya mali zake ingekuwa dhaifu.

Pili, kuundwa kwa masoko ya nchini kwa kutumia upana wa nguvu za dola. Historia inaonyesha kuwa uchumi wa soko una ufanisi mkubwa, kuliko soko hodhi.

Hata hivyo, uchumi huria halina uhakika, liahitaji kuundwa. China ilipoanzisha mageuzi yake kwenye masoko mwaka 1978, nchi ilikuwa kimsingi ilikiwa jamii yake ilikuwa ya wakulima (wakulima wadogo walikuwa asilimlia 82 ya wananchi wote).

Ni gharama kubwa kwa mkulima mdogo na asiye na elimu kuunda ushirika, isipokuwa kama kuna kuaminiana kijamii, huku kukiwapo soko.

Pia, ni gharama kubwa kuunda soko kubwa la pamoja kitaifa na soko la dunia kuisaidia mgawanyo wa kazi na uzalishaji mkubwa.

Na kwa upekee, ni kuna ghrama kubwa kuunda taasisi za udhibiti wa masoko, kuzuia udanganyifu na kughushi, lakini, CPC ilifaulu katika hilo!

Imekuwa iktumia mamlaka ya dola, kuondoa udhibiti wa kikanda na kuunda soko la pamoja kitaifa; imetunga sheria na kanuni za kuwaadhibu wadanganyifu, hata ikaweka muundo bura endelevu wa soko.

CPC, pia imefanikiwa kupata uanachama wa Shirika la Biashara la Dunia (WTO), ili wauzaji bidhaa nje kutoka China, wayafikie masoko ya nje.

Tatu; ni kufuata kwa usahihi mpangilio wa nchi ya viwanda. Maendeleo ya sokm la viwanda ni hatua ua mpangilio wenye mtiririko kutoka hatua ya kilimo na wabunifu viwanda wa ngazi ya chini (fundi mchundo), hadi soko la viwanda vidogo vinavyokua katika maeneo yanayochukua kasi ya maendeleo.

Hiyo inafika hadi kufikia uzalishaji mkubwa wa bidhaa za matumizi ya kawaida, kisha viwanda vikubwa vya kati vinavyounda vitendea kazi kama mashine na mwisho wale mifumo ya kisasa ya fedha na hatimaye taasisi na mifumo ya kisiasa.

Bila ya kujali nchi imechelewa kiasi gani kuanza uchumi wa viwanda, ni lazima irudie hatua za kwanza ndio ifikie mafanikio.

Njia ya China kufikia mapinduzi ya viwanda, ina hatua kuu o nne, na sasa iko katika safari ya hatua ya tano.

Nchi nyingi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, hazina serikali imara, hivyo zinakosa uwezo wa kuunda soko lake huru kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya uzalishaji mkubwa.

Baadhi yakei kama Somalia, Sudani Kusini na Jamhuri ya Afrika ya Kati, bado zinataabika na ugaidi, mapigano ya kikabila na vita vya wenyewe. Kutokuwapo kwa amani ya nyumbani, ni kikwazo kikubwa jitihada za uchumi wa viwanda katika nchi hizo.

Zaidi ya hapo, kuna nchi chache sana za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, zilizofuata mpangilio unaohitajika kufikia mapinduzi ya viwanda.

Nyingi bado zikio katika hatua za awali katika mapinduzi ya viwanda, jukumu kuu likiwa ni katika namna ya kuunda viwanda vya vijijini na vile ambavyo mfumo wake unaajiri zaidi nguvu kazi (labour intensive industries).

Hata hivyo, nchi nyingi za Afrika Kusini mwa la Sahara, zinaweka mkazo mkubwa katika ujenzi wa miundombinu au kuimarisha demokrasia, badala ya kujendeleza ujasiriamali vijijini, ambazo zinazaloisha bidhaa za kilimo na viwanda vinavoajiri zaidi kama vya mavazi.

Wakati CPC inasherehekea umri wa karne tangu kuanzishwa, sisi Waafrika tusiishie kupeleka salamu za pongezi kwa marafiki zetu wa China, lakini tujifunze kutoka walichopitia katika magezi ya viwanda kwa ustahimilivu.

Ni ndoto yangu kuwa siku moja Tanzania na nchi zingine za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, zitafikia mapinduzi ya viwanda na kufikia kasi ya uchumi duniani uliko, kama vile ilivyofanya katika miongo minne iliyopita.

- **Mwandishi ni Mhadhiri wa Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**



**Mistari kadhaa ya teknolojia ya glasi kuelezea ya mageuzi ya kiteknolojia iliyojengwa huko Shahe, Mkoa wa Hebei, maarufu Jiji la Kioo, nchini China.**



**Reli ya kisasa inayofanya kazi Tianjin North. Mnamo 2008, China ilianza rasmi kutoa hduma za usafiri wa reli ya kisasa katika kiwango cha kiwango cha kimataifa na inamiliki haki kamili za miliki.**



HABARI DODOMA

## Naibu Meya: Vijana shirikini shughuli za kuleta maendeleo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago, amewataka vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za kimaendeleo, ili kujikwamua kiuchumi.

Chibago aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na vijana wa Kanisa la Angalikan Parish ya Chamwino kwenye tamasha la kuchangia damu salama.

Aliwataka vijana kuibua miradi ya ujasiriamali ambayo itakayowawezesha kupata mikopo inayotolewa na halmashauri ili kukuza mitaji.

Aidha alisema ili kuipata mikopo hiyo inayotolewa na halmashauri wanatakiwa kuunda vikundi na kuibua miradi yenye tija.

Alisisitiza vijana wana wajibu wa kuhakikisha wanashiriki katika shughuli za kimaendeleo na kuchangia damu ili kuokoa maisha ya watu wenye uhitaji.

Alisema hospitali, vituo na zahanati vinahitaji damu salama, hivyo mfano ulioonyweshwa wa kujitolea kuchangia damu umegusa jamii.

"Kitendo kilichofanyika cha kuchangia damu salama kwa kupitia tamasha hili la uimbaji wa nyimbo za kiroho, kimegusa serikali na jamii, ukizingatia kuwa vituo vingi vya afya, zahanati na hospitali zetu zinauhitaji mkubwa wa damu," alisema.

Akisoma risala ya vijana Ofisa Maendeleo wa Dinary ya Chamwino, Alinikisya Humbo, alisema wao kama vijana wamejitokeza kuchangia damu ni sehemu ya kuiitikia wito wa serikali ambayo wa kuchangia damu kwa jamii.

**"Kitendo kilichofanyika cha kuchangia damu salama kwa kupitia tamasha hili la uimbaji wa nyimbo za kiroho, kimegusa serikali na jamii, ukizingatia kuwa vituo vingi vya afya, zahanati na hospitali zetu zinauhitaji mkubwa wa damu," alisema.**

# Umwagaji mafuta baharini sasa kudhibitiwa tena

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imefufua mpango wa kitaifa wa kudhibiti umwagaji wa mafuta baharini utakaosaidia kulinda mazingira na viumbe vingine, wakiwamo samaki na kuimarisha uchumi wa bluu.

Mkurugenzi wa Usalama na Mazingira Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Stella Katondo, alibainisha hayo jana jijini hapa kwenye kikao na wadau juu ya mpango wa kitaifa wa kupambana na umwagikaji wa mafuta baharini.

Katondo, alisema lengo la mpango huo ni kusaidia kupambana na umwagikaji wa mafuta kwenye bahari pamoja na maziwa makuu.

Alisema mpango huo ulikuwapo tangu mwaka 2016, lakini hivi sasa umefufuliwa kutokana na mabadiliko mbalimbali yalivyojitokeza katika sekta hiyo.

"Awali mpango huu ulikuwa chini ya Sumatra, lakini kutoka na Sumatra kuvunjwa serikali iliamua kuuleta katika Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) ili kuweza kuutekeleza kwa kushirikiana na wadau wengine," alisema Katondo.

Vile vile, alisema Tanzania ni moja kati ya nchi zinazohusika katika usafirishaji baharini na kwenye maziwa makuu, na vyombo hivyo vinatumia mafuta na vinabeba mizigo ya nishati hiyo mpango huo utasaidia kuwapo na namna nzuri ya kusafisha pale yanapovuja.

"Mpango huu utasaidia kuwa na vifaa ambavyo vitatumika kuondoa au kusafisha mafuta pindi yanapovuja baharini au katika maziwa makuu ili kuokoa mazingira pamoja na viumbe vilivyomo kama samaki," alisema.

Aidha, alisema kitendo cha kuvunja kwa mafuta baharini kina athari kubwa kwa viumbe vilivyomo, hivyo ni lazima iwapo namna sahihi ya haraka kuyaondoa katika eneo hilo.

Akizungumzia hali ya umwagikaji wa mafuta baharini kwa hivi sasa, alisema si mbaya kutokana na udhibiti unaofanywa katika vyombo vya usafirishaji kama vile meli na boti.

Kaimu Msajili wa Meli, Mhandisi Alfred Waryana, alisema kuwa mpango huo utasaidia taifa kuwa na vifaa vya kisasa vya kusafisha na kuondoa mafuta yanapovuja baharini katika vyombo vya usafirishaji.

"Lakini mpango huu utawezesha kusaidia kupata msaada kwa mataifa mengine yenye vifaa vya kisasa pale linapotokea janga kubwa la kuvunja kwa mafuta baharini ili kusaidia kuyaondoa kabla ya kuleta athari kubwa kwa viumbe, pia mpango huu utasaidia kujenga ushirikiano na mataifa mengine," alisema. Mhifadhi, ufundi na uwezeshaji wa hifadhi za bahari, Clever Mwaikambo, aliishukuru serikali kwa kufanikisha kupatikana kwa mpango huo ambao utakuwa mkombozi wa mazingira na kulinda uchumi wa bluu.

Alisema kuwa ni lazima taifa kuwa na vifaa vya kusafisha na kuondoa mafuta pale yanapovuja baharini ili mazingira kuendelea kubaki salama pamoja na viumbe vilivyomo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Sera, Kazi, Vijana na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (wa pili kulia), akikabidhi zawadi kwa Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi iliyotolewa na Chama cha Wabunge Wanawake (TWGP), ikiwa ni ishara ya kumpongeza kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo, jijini Dodoma juzi. Watatu kulia ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# CCM: Tunataka mipango ya serikali yenye majibu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kinahitaji kuona mipango ya serikali yenye kuleta majawabu kwa vitendo.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wadau kutoka katika taasisi za uwezeshaji mkoani Dodoma.

Shaka alisema mipango hiyo imekuwa ikiainisha malengo mazuri kwa kila mwaka, lakini utekelezaji wake ni mdogo.

Alisema wakati umefika kuweka na mpango shirikishi kwa wadau hao na uwekewe uratibu mzuri wa kufanyiwa tathmini kila baada ya muda.

"Tuna wajibu wa kuleta uhuru wa kiuchumi na kuhakikisha nchi yetu inajenga uchumi wa kisasa, ambao sio tegemezi kupitia mapinduzi ya kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda kwa kutumia teknolojia. Kazi kwetu kuamua kutekeleza wajibu huo," alisema Shaka.

Alisema sifa ya CCM inataka kuwa na fikra na vitendo vya kimapinduzi na zinalenga kuleta maendeleo na mabadiliko makubwa na ya haraka katika nchi.

"Hili linawezekana ikiwa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi zitakuwa na bajeti, mipango shirikishi, utaratibu usio na urasimu pamoja na masharti magumu, inafahamika au kupatikana kirahisi, ina mchakato wa wazi wa utoaji mikopo au vitendea kazi, ina mfumo mzuri wa kuwasimamia vijana wakati wote wa utekelezaji wa miradi ili kupata matokeo yaliyotarajiwa," alisema Shaka.

Shaka alisema ilani ya uchaguzi ya CCM imeahidi upatikanaji wa ajira milioni nane katika kipindi cha miaka mitano, hivyo CCM inahitaji majawabu halisia kwa kila taasisi ya umma namna alivyotekeleza sambamba na kuainisha mikakati iliyojiwekea ambapo chama kitapita kukagua na kujiridhisha.



# Wakulima mpunga walamba ruzuku mil. 478/-

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa mpunga katika Kijiji cha Azimio, Mbarali mkoani Mbeya, wametia saini mkataba na Kampuni ya USADF ya Marekeni kwa ajili ya kupatiwa ruzuku ya Sh. milioni 478 ili kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao yao.

Mkataba huo wa miaka minne ulitiwa saini uzi kati ya Mratibu wa Shughuli za USADF, Gilliard Nkini na viongozi wa kampuni ya wakulima wa mpunga wa kijiji hicho.

Akizungumza wakati wa kutia saini mkataba huo, Nkini alisema lengo la kutoa ruzuku hiyo ni kuongeza ubora wa mazao yanayozalishwa na wakulima wa kijiji hicho ili kuinua uchumi wao na kuwa na uhakika wa chakula.

Nkini alisema si mara ya kwanza kwa taasisi hiyo kuwasaidia wakulima kwa kuwa awali ilitoa ruzuku ya Sh. milioni 200 mwaka 2016 na baada ya kuona wamefanya vizuri, iliamua kuongeza kiwango.

"Fedha hizi ni kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao. Mkuu wa USADF, Elizabeth Feleki, ameridhishwa na kazi yenu ndiyo maana ameamua kuwaongezea ruzuku na hii ruzuku itatolewa mpaka mwaka 2024," alisema.

Viongozi wa Kampuni ya Wakulima ya Azimio Mswiswi High Quality Rice Millers yenye zaidi ya wakulima 300, walisema mbali na wanachama wao kunufaika na ruzuku hiyo pia na vijiji vingine saba vya jirani vitanufaika.

Katibu wa Kampuni hiyo, Luquman Shirima, alisema watazitumia fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa ghala la kisasa la kuhifadhia mazao pamoja na kununua mashine ya kisasa ya kukoboa mpunga.

Alisema watazitumia pia kuongeza mtaji wa wakulima ili kuhakikisha wanaongeza uzalishaji na kufikia hatua ya kujitegemea endapo wafadhili wataacha kuwapelekea fedha za kuendeleza shughuli za kampuni yao.

"Tunashukuru kampuni hii kwa ruzuku hii. Wakulima tutaongeza uzalishaji na kuongeza ubora wa mazao yetu. Kwa sasa tutaongeza nguvu ya kutafuta soko la mazao yetu ili wakulima wanufaike zaidi," alisema Shirima.

Baadhi ya wakulima wa mpunga, waliiomba serikali iwasaidie kuboresha miundombinu ya barabara ili wawe wanasafirisha vizuri mazao yao kutoka shambani kwenda kwenye maghala pamoja na kusafirisha pembejeo kwenda mashambani.

Mmoja wa wakulima hao, Andrea Mwambenengo, alisema kutokana na ubovu wa barabara za eneo hilo baadhi ya magari makubwa yamekuwa yakishindwa kuingia na kutoka wakati wa kusafirisha mazao, hivyo kulazimika kutumia matrekta.

Alisema watashirikiana na viongozi wao kuendelea kuiomba serikali iwaboreshee miundombinu hiyo ili wasafirishe mazao yao kwa urahisi zaidi.

Mbarali ni miongoni mwa wilaya za Mbeya ambazo uchumi wa wananchi wake unategemea zaidi kilimo cha mpunga.




Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Saitoti Zerote (katikati), akiwakabidhi viongozi wa vikundi 23 mfano wa hundi ya Sh. milioni 449, kwa ajili ya mkopo unaotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Vijana wapewa mchongo ajira kimataifa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA wameshauriwa kuchangamkia fursa zinazotangazwa kwenye jumuiya mbalimbali za kimataifa ikiwamo Jumuiya ya Nchi za Bonde la Mto Nile ili kuonyesha uwezo wao wa kufanya kazi na kupunguza tatizo la ajira.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, aliyasema hayo jana alipokuwa anazungumza na Nipashe akiwa nchini Ethiopia ambako aliiwakilisha Tanzania kwenye Mkutano wa 24 wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Nchi za Bonde la Mto Nile.

Alisema Tanzania ina vijana wengi wenye uwezo wa kufanya kazi kwenye jumuiya hiyo lakini wamekuwa hawajitokezi kutokana na kutofuatilia taarifa za kimataifa.

Alisema katika mkutano huo, mawaziri wa nchi tisa kati ya 10 za Ukanda wa Maziwa Makuu, walikubaliana kuwahamasisha vijana kutoka kwenye mataifa yao kuwa wepesi wa kufuatilia taarifa za muungano wa mataifa mbalimbali.

"Vijana wetu wa kitanzania wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi lakini tatizo lao huwa ni ufuatiliaji wa hizi taarifa za muungano wa mataifa zaidi ya moja. Sasa ni wajibu wetu kuwahamasisha vijana wetu kufuatilia taarifa hizi," alisema Mahundi.

Alisema katika mkutano huo ambao ulitanguliwa na maofisa bonde wa Bonde la Mto Nile, Mtanzania Mwasiti Rashidi aliteuliwa kuwa Mratibu wa Vyanzo vya Maji, Utawala na Maendeleo wa Sekretarieti ya Bonde hilo.

Mahundi alisema kabla ya uteuzi huo, Rashidi alikuwa ofisa wa kawaida kwenye sekretarieti hiyo na kwamba ana uhakika kwamba ataiwakilisha vizuri Tanzania na atasaidia kufungua fursa kwa vijana wengine wa kitanzania.

Pia alisema kwenye mkutano huo walisisitiza kuhakikisha nchi zote za Bonde la Mto Nile zinanufaika na miradi mbalimbali inayotekelezwa kwenye bonde hilo ikiwamo kufua umeme ambayo alidai inazalisha pia ajira kwa vijana.

Alisema mikutano hiyo wakati mwingine huwa inasaidia kujenga diplomasia ya kiuchumi kwa nchi zote za bonde hilo na kuibua fursa zingine za kiuchumi.

Hata hivyo, alisema kutokana na uwapo wa janga la virusi vya corona, ni vyema mataifa ya ukanda huo kutumia wataalamu wa ndani kutekeleza miradi mbalimbali na kwamba utaratibu huo utasaidia kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa miradi hiyo.

Aliyataja mataifa ambayo yalishiriki mkutano huo kuwa ni Tanzania, Burundi, Ethiopia, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Sudan, Sudani Kusini, Uganda, Kenya. Misri ndilo taifa pekee ambalo halikushiriki.

# Wabomoa kilabu kujenga zahanati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mtaa wa Ndanyela, Kata ya Nzovwe jijini Mbeya, wamekubaliana kuvunja kilabu cha pombe za kienyeji kilichokuwapo mtaani hapo na kulitumia eneo hilo kujenga zahanati.

Uamuzi huo umetokana na kutokuwa na sehemu nyingine kwa ajili ya ujenzi wa taasisi hiyo.

Wakizungumza wakati wa kubomoa kilabu hicho jana asubuhi, wakazi hao walisema wameshapokea Sh. milioni 250 kutoka serikalini kwa ajili ya ujenzi wa zahanati, hivyo wakaona eneo sahihi la kujenga ni mahali hapo.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Philip Mwalindu, alisema kilabu hicho kilijengwa mwaka 1963 lakini kilikuwa kero kwa wakazi wa eneo hilo kutokana na kuwa chanzo cha uhalifu.

Alisema kwa muda mrefu wananchi hao walikuwa wanatafuta sababu ya kuvunja kilabu hicho, lakini wakawa hawaipati baada ya kupata fedha hizo, wakaona ni wakati sahihi wa kufanya hivyo.

"Nguvu kazi ya vijana wetu imekuwa ikipotea hapa. Vijana wamekuwa wakinywa pombe hata asubuhi, hivyo kutofanya kazi. Kwa hiyo tuliitisha mkutano ambao wananchi waliridhia kukivunja kilabu hiki na kujenga zahanati ili angalau tuwanusuru vijana wetu," alisema Mwalindu.

Diwani wa Nzovwe, Mchungaji David Mwashilindi, tayari fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa zahanati hiyo zimefika, hivyo wananchi hao wanatakiwa wafanye maandalizi mapema ya kujenga.



# Hali ya biashara yaongezeka kwa 53.8%

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Divisheni ya Takwimu za Watoaji Huduma kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Bakari Khamis Kondo, amesema hali ya biashara kwa mwezi Mei, mwaka huu, imeongezeka kwa asilimia 53.8 ikilinganishwa na mwezi Mei, mwaka 2020 huku ikipungua kwa asilimia 15.0 ukilinganisha na mwezi Aprili, mwaka huu.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa tathmini na mwenendo wa hali ya biashara kwa mwezi wa Mei mwaka huu huko ofisini kwake Mazizini Mjini Unguja.

Alisema mwenendo wa biashara bado unaendelea kuwa katika hali nzuri na kuongezeka kwa asilimia 53.8 ikilinganishwa na mwezi Mei, mwaka jana.

Pia alisema, hali hiyo inachangiwa na mambo mbalimbali na kwamba kwa makadirio ya fedha ni Sh. bilioni 70.5 huku thamani nzima za bidhaa zilizosafirishwa kutoka Zanzibar kwenda nje ya nchi zilikuwa na thamani ya Sh. bilioni 2.9.

"Kwa thamani ya bidhaa zilizosafirishwa zimeongezeka kwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na mwezi Mei 2020 na kwa asilimia 19.5 ikilinganisha na mwezi Aprili 2021," alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa bidhaa zilizosafirishwa ni pamoja na chakula, wanyama hai bidhaa zilizotengenezwa aina ya malighafi, vifaa ghafi vya nishati ya mafuta, mashine na vifaa vya usafirishaji, bidhaa za viwandani pamoja na kemikali.

Kwa upande wa usafirishaji wa bidhaa kwa nchi tano bora kwa mwezi Mei, mwaka huu umefikia asilimia 70.6 ya bidhaa zote zilizosafirishwa.

"Nchi ya Denmark imeongoza kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya Sh. milioni 620 sawa na asilimia 21.0," alisema.

Alisema katika nchi nyingine zinazoongoza katika usafirishaji wa bidhaa ni Vietnam, China, India na Uganda na bidhaa kuu zilikuwa mwani, pumba, samaki aina ya kaa, kamba na kobe.

Alisema kuwa Zanzibar kwa mwezi Mei mwaka huu bidhaa zilizosafirishwa nje ya nchi zilikuwa mitumba ya nguo, vyuma chakavu, vitenge, kanga pamoja na vikoi ambapo bidhaa zilizoagizwa kwa mwezi Mei mwaka huu zinathamani ya Sh. bilioni 73.5.

"Thamani ya bidhaa zilizoagizwa zimeongezeka kwa asilimia 51.3 ikilinganishwa na mwezi Mei mwaka 2020 na asilimia 15.2 ikilinganishwa na mwezi Aprili, mwaka huu," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa kundi la mafuta, vilainishi na vifaa vinavyohusiana limechangia asilimia 47 ya bidhaa zote zilizoagizwa kama vile mashine na vifaa vya usafirishaji, chakula na wanyama hai, bidhaa za viwandani, vinywaji na tumbaku.

Alisema, uingizaji wa bidhaa kwa nchi tano zilioongoza umefikia asilimia 76.0 ya thamani ya uingizaji wote kwa mwezi Mei 2021.

"Nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu zimeongezeka kwa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 40.3 sawa na asilimia 54.9," alisema.

Katika uingizaji wa bidhaa kwa nchi tano ni Falme za Kiarabu, India, China, Malaysia na Spain.




Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui (kulia), akipokea boksi la vifaa vya usajili kwa ajili ya chanjo ya kipindupindu inayotarajiwa kutolewa kuanzia Julai 3 hadi 7 katika shehia 56 ambazo huathirika na maradhi ya kipindupindu mara kwa mara, ofisini kwake Mnazimmoja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Kila mwananchi atokomeze udhalilishaji'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto Zanzibar, Haroun Ali Suleiman, amesema umefika wakati wa kila mmoja kuwajibika ipasavyo ili kutokomeza vitendo vya udhalilishaji nchini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kamati hiyo mjini hapa, Waziri Haroun, alisema tatizo la udhalilishaji linaendelea kukemewa vikali na serikali pamoja na wadau mbalimbali na nguvu ya pamoja inahitajika ili kutokomeza tatizo hilo.

Alisema lengo la kikao hicho kilichoshirikisha wadau mbalimbali wa udhalilishaji ikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama ni kukusanya maoni ya wadau ambayo yatasaidia kupanga mikakati madhubuti ya kupambana na udhalilishaji nchini.

Alisema, vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa watoto vinadumaza ustawi wa jamii na maendeleo ya watoto wengi nchini.

"Hivi sasa tunataka tumalize kabisa vitendo hivi ili iwe ni historia kwa Zanzibar visiwepo tena, vimetutosha watoto wetu bado wanadhalilishwa sasa udhalilishaji basi," alisema.

Aliipongeza serikali kwa kuanzisha mahakama maalum ya udhalilishaji ambayo itasaidia kuongeza jitihada za kumaliza udhalilishaji nchini.

# Wakulima watakiwa kuchangamkia mazao ya viungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKULIMA wametakiwa kuchangamkia fursa zinazopatikana na kujikita katika kilimo cha mazao ya viungo ambacho bei yake ni nzuri yenye tija katika soko la dunia.

Meneja mradi wa viungo kanda wa Unguja, Khadija Juma, alisema hayo jana wakati akishiriki katika kazi za ugawaji wa mbegu za mazao ya vanilla, Kizimbani Mkoa wa Magharibi, Unguja.

Alisema mradi wa viungo umejikita kuwawezesha wakulima kulima mazao ya aina mbalimbali na kuwapatia mapato ambayo yatasaidia kujitegemea kufuatia mradi huo kulenga wanawake asilimia 55.

"Huu ni mradi muhimu ambao umelenga kuwafikia wakulima 57,974 huku asilimia 55 ni wanawake hatua ambayo itawafanya kujikomboa na kujitegemea," alisema.

Mkulima wa kilimo cha mazao ya vanila, Haji Abdalla Abeid, alisema alikuwa akilima vanilla, lakini kwa njia ya kienyeji zaidi baada ya kupata elimu na utaalamu kutoka kwa mabwana shamba sasa anatumia mbinu za kitaalamu.

Alisema kilimo cha viungo cha vanila wastani wa mavuno yake kwa mwaka mara moja na kinastawi vizuri katika maeneo ya kisiwa cha Unguja na Pemba katika ardhi yenye udongo.

"Matarajio yangu makubwa sasa kulima kilimo cha mazao ya viungo cha vanila kwa mafanikio makubwa na kuingia katika soko la Afrika ya Mashariki kwa kuuza bidhaa," alisema.

Ali Juma Seif, msimamizi wa mradi wa mazao ya viungo ikiwamo vanila, alisema kilimo hicho kwa sasa ndiyo mkombozi wa wakulima kutokana na bei yake nzuri yenye tija.

Alisema, katika soko la kimataifa kilo moja ya vanila hivi sasa inauzwa kati ya Sh. milioni 1.6 huku soko kubwa lipo katika nchi za Ulaya na Asia.

"Kilimo hiki kama wakulima watalima kwa kufuata masharti yanayotokana na mabwana shamba pamoja na mabibi shamba watakuwa wamepiga hatua kubwa na kujikomboa katika ukulima duni na kuingia katika biashara ya usafirishaji wa mazao ya kilimo na viungo," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI YA KAZI

Nafasi za Kazi ya ualimu diploma science na hesabu 0783298900

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTEA KWA CHETI



**IRENE ENOCK KITINGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S **2549-0532** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ALPHA mwaka 2014,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/326586/2021**

116339002

## KUPOTEA KWA VYETI



**NEEMA MOSES MBILINYI** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba **S 2295/0051** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MAIRIVA mwaka 2014,na certificate yenye namba **BTCA/0762/t.2016** mwaka 2016 na cheti cha DIPLOMA chenye namba **ODA/1368/t.2017** mwaka 2017,vilivyotolewa na chuo cha INSTITUTE OF ACCOUNTANCY ARUSHA,yeyote atakayeviokota atoe taarifa polisi
Polisi taarifa **DAR/CHA/RB/305333/2021.**

116339402

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334), KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI.**

**HATI NAMBARI:53491**

**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: MATHAYO SHAMBA LABOWA**

**ARDHI: KIWANJA NA 842 & 844 KITALU "NN" Maisaka Katani BABATI MJINI.**

**MUOMBAJI: MATHAYO SHAMBA LABOWA WA S.L.P 575 BABATI.**

**TAARIFA IMETOLEA** kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa mwezi mmoja (1) tokea tarehe ya taarifa hii.

Iwapo Hati ya asili ikionekana, irudishwe kwa Msajili wa Hati Msaidizi Mkoa wa Manyara, S.L.P 621, BABATI – MANYARA.

EDWARD M'AKORI
MSAJILI WA HATI MSAIDIZI

**Tarehe: 28 Juni, 2021**

116339502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MOROGORO MOROGORO**

**SHAURI LA MADAI NA. 44 YA 2019**

**MUSTAKIM A. SADICK ............MSHINDA TUZO**

**DHIDI YA**

**OMARY IBRAHIM ...............MSHINDWA TUZO**

**WITO WA MAHAKAMA**

**KWA: OMARY IBRAHIM**
Wito huu ni wa kesi tajwa hapo juu, ambayo imepangwa kujatjwa kwa utekelezaji tarehe 08 mwezi 07 mwaka 2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mahakama Hakimu Mkazi Morogoro.
Unatakiwa kuhudhuria wewe binafsi au wakili au mtu yeyote aliyeidhinishwa kusimama kwa niaba yako na pia unatakiwa kutoa maelezo yako ya siku hiyo nakala zote za ushahidi utakazo zitumia kwa nini utekelezaji usiendelee dhidi yako.
Zingatia kwamba, kutohudhuria siku ya kesi na kwa wakati uliotajwa hapo juu, Mahakama itaendelea na kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila ya uwepo wako.
Imetolewa chini ya muhuri wa Mahakama leo siku ya tarehe 29 mwezi 06 mwaka 2021.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MOROGORO

116339701

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI ARUSHA**

**MAOMBI YA JINAI NA 18 YA MWAKA 2020**

**DIRECTORS OF PUBLIC PROSECUTION.........MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ZAINABU MZIRAY..........,MJIBU MAOMBI**

**EMMANUEL ALEX MASOME............MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**TO.EMMANUEL ALEX MASOME.**

**DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTION** ameasilisha shauri la maombi ya jinai ya kesi namba 18 kutajwa tarehe 6/07/2021 saa 3:00 kamili asubuhi.hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuhudhuria bila kukosa. Endapo hautatekeleza ,maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.

Imetolewa na kutiwa muhuri na mahakama ya hakimu mkazi leo tarehe 11/6/2021

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI ARUSHA.
HAKIMU MKAZI
ARUSHA

116340002

**KATIKA MAHAKAMA KUU TANZANIA DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA 64 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU SYLVESTER JOSEPH SAWAKI MWOMBAJI/WAOMBAJI JOVIN SYLVESTER SAWAKI & NATALIA SYLVESTER SAWAKI**

**TAARIFA YA KAWAIDA (kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaonainafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitsho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 20th mwezi july 2021

Imewasilishwa leo dar es salaam tarehe 18th mwezi june 2021

NAIBU MSAJILI

116339302

## BISMILLAH RAHMAN RAHIM

Familia ya marehemu **DK.Omar Ali Juma** inapenda kuwakaribisha kwenye hitima ya kumuombea marehemu DK.Omar Ali Juma itakayofanyika siku ya jumapili tarehe 4 julai,2021 saa kumi jioni katika msikiti wa Ngazija. Kufika kwenu ndio mafanikio yetu.ndugu ,marafiki na jamaa wote mnakaribishwa.

**Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi.**

**Amin.**

*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa Kwa*

*Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# CBE yapigia debe kozi viwango na vipimo

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimewataka vijana kuchangamkia kozi ya vipimo na viwango inayotolewa na chuo hicho kwa kuwa ina wigo mpana wa ajira.

Hayo yalisemwa jana na Mhadhiri Msaidizi wa Idara ya Vipimo na Viwango wa chuo hicho, Ishigata Lucas, kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Alisema fani hiyo bado haijachangamkiwa na watu wengi kutokana na kutoifahamu lakini vijana wengi wanaohitimu wamekuwa wakiajiriwa moja kwa moja na taasisi kama Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Vipimo (WMA).

Lucas alisema kozi hiyo ilianza mwaka 1978 chuoni hapo lakini bado haijachangamkiwa na watu wengi kama fani za uhandisi, hivyo vijana wanapaswa kuiona hiyo kama fursa kwao kwa kuwa soko la ajira si la kutafuta kama wa fani zingine.

"Mahitaji ya wataalamu wa vipimo na viwango ni makubwa sana. Kwa mfano mwaka huu WMA ilitaka kuajiri wataalamu wa vipimo 300 lakini imeajiri 150 tu kwa sababu ndio waliopo na malengo yao hata wangekuwapo 600 wangewaajiri tu, hivyo soko lipo," alisisitiza.

Pia alisema mbali na fursa kubwa ya kuajiriwa na TBS na WMA, wahitimu wa fani hiyo wanaweza kuajiriwa kwenye viwanda mbalimbali kwa ajili ya masuala ya vipimo na viwango.

Lucas alisema CBE ni chuo pekee kwa nchi za Afrika Mashariki (EAC) na Kusini mwa Afrika (SADC) inayotoa kozi ya vipimo na viwango.

Alisema wahitimu wa kozi hiyo wana fursa ya kuajiriwa pia kwenye mataifa hayo ambako nako idadi ya wataalamu hao ni ndogo sana kulinganisha na mahitaji yao.

CBE, alisema imekuwa ikitoa wahitimu 40 mpaka 50 wa fani hiyo idadi ambayo alisema ni ndogo sana kulinganisha na fani zingine kama uhandisi.

"Vijana wengi wanakimbilia fani ya uhandisi lakini sisi tunawaambia wengine waje kwenye utaalamu wa vipimo na viwango nako kuna fursa nyingi tu za ajira. Wasifikirie fani hizo tu kwamba ndizo zinaajiri sana," alisema.

# Mbunge: Samia ameonyesha mwanga siku 100 Ikulu

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Morogoro Mjini (CCM) Abdulaziz Abood, amepongeza kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ndani ya siku 100 akiwa rais kuwa ni ya kipekee.

Akizungumza jana, Abood alisema ndani ya siku 100 Rais Samia ameonyesha mwelekeo sahihi wa nchi kwa jitihada zake za kufungua milango ya uchumi na kuimarisha mifumo ya serikali.

Abood alisema kama Rais Samia amefanya mambo makubwa kama haya ndani ya siku 100 basi Watanzania watarajie mambo makubwa mazuri siku za usoni na wampe ushirikiano ili aweze kutimiza malengo yake.

"Tumepata kiongozi mwenye maono, mwadilifu na mchapakazi ambaye atajjenga nchi hadi kufikia uchumi wa juu kinachotakiwa ni kumpa nafasi na ushirikiano ili atimize ndoto zake," alisema.

Mbunge huyo alisema Rais Samia ni mtulivu, msikivu na anayejali utawala wa haki, demokraaia na utawala wa sheria mwelekeo ambao umewavutia Watanzania wengi wa rika zote.

Alisema hakika Tanzania imempata kiongozi ambaye atailetea maendeleo makubwa kutokana na kufanya vyema ndani ya kipindi kifupi cha siku 100.

"Tumeshuhudia namna ambavyo amekuwa na upendo kwa kukaa na kuzungumza na makundi mbalimbali kama wazee, vijana, wanawake na viongozi wa dini hii inatupa dalili njema kwamba kiongozi tuliye naye ni sahihi," alisema.

Aisema Watanzania wa rika mbalimbali wamepongeza siku 100 za Rais Samia madarakani hali inayoonyesha kwamba kiongozi huyo anaungwa mkono na asilimia kubwa ya watu.

Pia alisema hatua ya Rais Samia kushirikisha kwa karibu sekta binafsi kwa kuvutia uwekezaji mpya kutafungua milango ya uchumi kwa haraka sana.

Alisema mwelekeo huo mpya wa serikali yake kuondoa urasimu kwenye sekta binafsi kumesababisha mafuriko ya wawekezaji ndani ya muda mfupi.

"Ninachosisitiza tumpe nafasi na tumpe ushirikiano ili atimize majukumu yake, kuna miradi mingi ya kimkakati inaendelea na chini ya usimamizi wake mahiri nina imani kubwa kwamba itamalizika kwa wakati, " alisema Abood.




Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya kutengeneza na kusambaza mbolea ya Yara Tanzania, Winstone Odhiambo (wapili kulia), Bwana Shamba Mwandamizi wa Yara, Maulidi Mkima (kushoto), Meneja Masuluhisho ya Kidigitali wa Yara, Deodath Mtei na Meneja Masoko, Sheila Chatto wakifurahia baada ya uzinduzi wa programu maalum iitwayo 'YaraConnect APP', jijini Dar es Salaam jana, yenye lengo ya kutoa elimu ya kitaalamu kuhusu kilimo kwa wateja watakaojisajili. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mpango kuwafikia wakulima waanza

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kutengeneza na kusambaza mbolea ya Yara imezindua programu maalumu iitwayo 'YaraConnect APP' ikiwa na malengo ya kutoa elimu ya kitaalamu kuhusu kilimo kwa watakaojisajili.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa programu hiyo, jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema uzinduzi wa YaraConnect ni moja ya malengo yao katika kubuni mbinu sahihi za kitaalamu katika kilimo ikiwamo za njia ya kidijitali.

Alisema Yara ni kampuni inayojihusisha na utengenezaji na usambazaji wa mbolea Tanzania kwa takribani miaka 15, ikiongoza duniani kwa uzalishaji na usambazaji wa mbolea, utunzaji wa mazingira na kutoa suluhisho la kitaaluma kuhusu uzalishaji wa mazao mbalimbali.

"Hii ni 'App' mpya kabisa itakayopatikana kwa kupitia simu za 'smart' na inalenga wauzaji na wasambazaji wa bidhaa za Yara, watumiaji wa simu za kupangusa," alisema.

Aliongeza kuwa wasambazaji na wauzaji wa mbolea ya Yara wanaweza kutumia 'App' hiyo kusajili biashara zao mara moja na kujizolea pointi kwa kupiga picha alama maalumu kutokana na manunuzi ya bidhaa za Yara huku wakipata taarifa kuhusu pointi zao na kutumia pointi hizo wanapotaka kujizolea zawadi zao mbalimbali kama pikipiki, simu, pesa taslimu na zawadi nyinginezo.

Aidha, alisema wasambazaji pia watajifunza kupitia video za maarifa zipatikanazo ndani ya 'App' na kujua maswali yanayoulizwa sana na wakulima wa eneo husika ambapo watumiaji watapata nafasi ya kupata msaada wa kitaalamu kuhusu lishe linganifu kwa mimea kupitia 'App' hiyo.

# MBAPPE AKATAA MKATABA MPYA PSG



**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe ameitaarifu Paris-Saint Germain kuwa hana mpango wa kusaini mkataba mpya, kwa mujibu wa L'Equipe.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 raia wa Ufaransa, kwa sasa hataki kuongeza mkataba mpya wa kuendelea kuwachezea miamba hao wa jijini Paris.

Mkataba wa sasa wa Mbappe unatajiwa kumalizika 2022 na PSG imekuwa ikihaha kuhakikisha nyota huyo anabaki klabuni hapo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya L'Equipe, Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi, yupo kwenye harakati za kumshawishi Mbappe kuongeza mkataba wake na klabu hiyo.

Rais Al-Khelaifi kwa sasa ameamua kuchukua jukumu la Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Leonardo kwa ajili ya kumshawishi Mbappe kubaki klabu hapo.

Mapema mwezi uliopita, rais huyo alibainisha wazi kwamba, hawana mpango kabisa wa kumuuza Mbappe kipindi hiki cha majira ya joto.

Klabu ya Real Madrid imekuwa mstari wa mbele kuwania saini ya Mbappe kwa muda mrefu sasa na yeye mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kwenda kucheza kule Santiago Barnabeu.

Liverpool pia imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka saini ya nyota huyo ambaye alishinda Kombe la Dunia na Ufaransa mwaka 2018 nchini Urusi.

# Sancho rasmi mali ya Man United

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imefikia makubaliano ya ada kiasi cha Euro milioni 85 na Borussia Dortmund kwa ajili ya kumsajili, Jadon Sancho.

Winga huyo wa England mwenye umri wa miaka 21, ambaye bado hajafanyiwa vipimo vya afya yake na makubaliano ya maslahi binafsi, anatarajia kusaini mkataba wa miaka mitano na kipengele cha kuongeza mmoja.

Ada hiyo italipwa kwa mafungu mara tano, na itamfanya Sancho kuwa mchezaji wa pili ghali zaidi wa Uingereza nyuma ya Harry Maguire.

Mlinzi Maguire alijiunga na United akitokea Leicester kwa ada ya pauni milioni 80 mwaka 2019.

Manchester City ambayo ndio klabu yake mama, itapata faida ya asilimia 15 ya mauzo ya Sancho kutoka Dortmund.

Sancho alijiunga na miamba hao wa Bundesliga kwa pauni milioni 10 miaka minne iliyopita.





# Morata: Najua sababu mashabiki kunizomea

**SEVILLE,** Hispania

ALVARO Morata amesema anajua kwa nini amekuwa akizomewa kwenye michuano ya Euro 2020, lakini hajajiandaa kuzungumzia sababu hadi Hispania itakapomaliza michuano hiyo.

Straika huyo wa Juventus amefunga mabao mawili kwenye michuano hiyo, likiwamo moja lililokifanya kikosi hicho cha Luis Enrique kurudi kwenye uongozi kipindi ca muda wa ziada wakati wakishinda mabao 5-3 dhidi ya Croatia kwenye hatua ya 16-bora.

Wakati huo huo, Morata alikosa nafasi nyingi za kufunga na hadi sasa ndiye mchezaji anayeongoza kwa kukosa nafasi nyingi zaidi za kucheka na nyavu kwenye michuano hiyo ikiwa ni mara sita.

Na sasa atakuwa na nafasi nyingine kwenye mchezo wa robo fainali wakati Hispania itakapocheza na Uswisi leo, Ijumaa.

"Najua sababu (kwa nini wananizomea mimi)," alisema akiiambia Deportes Cuatro. "Najua vizuri sana na si ngumu kuelewa.

"Wakati michuano ya Ulaya itakapomalizika, na kama mambo yanakwenda vizuri, nitazungumza. Sina tatizo. Najua vizuri sana kwa nini wananizomea."

# Daka wa Zambia asajiliwa Leicester

**LONDON,** England

NYOTA wa Zambia aliyekuwa anaichezea klabu ya Salzburg ya nchini Austria, Patson Daka, amesajiliwa rasmi na timu ya Leicester City ya England.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amesajiliwa kwa kitita cha pauni milioni 23 baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia msimu uliopita.

Daka alianza kucheza soka mwaka 2014 akichezea Kafue Celtic ya huko Zambia.

Mwaka 2015, Daka alicheza mchezo wa kwanza akiwa na timu ya Taifa ya Zambia na mwaka 2017 alifanikiwa kufunga bao la kwanza kwa timu hiyo kabla ya kushinda tuzo ya mchezaji bora kijana wa mwaka wa Shirikisho la Soka la Afrika, CAF.

Daka alijiunga na Red Bull Salzburg ya Austria ambapo aliisaidia kushinda taji la Ligi Kuu ya nchini hiyo maarufu kama Bundesliga akiwa na mwaka mmoja tu tangu ajiunge nayo mwaka 2018.

Akiwa na Salzburg, Daka amefanikiwa kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kushinda tuzo ya mchezaji bora wa Ligi Kuu Austria, Bundesliga, huku akimaliza msimu wa 2020/21 akiwa kama mfungaji bora wa ligi hiyo.

Baada ya kutangazwa, Patson alieleza kuwa anafurahia sana kusajiliwa katika klabu hiyo ambayo amekuwa akiifuatilia toka ichukue ubingwa wa EPL mwaka wa kwanza katika Ligi Kuu England.






# BENITEZ KOCHA MPYA EVERTON

**LONDON,** England

RAFAEL Benitez ametambulishwa rasmi kuwa kocha mpya wa Everton baada ya Muitaliano Carlo Ancelotti kutimkia Real Madrid.

Benitez amepewa mkataba wa miaka mitatu huku mmiliki wa timu hiyo, Farhad Moshiri, akisisitiza kuwa ni chaguo bora kwa klabu hiyo katika kuiletea mafanikio.

Duncan Ferguson, ataendelea kusalia klabuni hapo kama sehemu ya safu ya timu ya Benitez pamoja na kocha wa magolikipa Alan Kelly.

Kocha huyo wa zamani wa Liverpool mwenye umri wa miaka 61, alikumbana na changamoto kubwa kutoka kwa mashabiki wa timu hiyo kwa kile walichodai kuwa ni asili ya Liverpool ambao ni wapinzani wao wa jiji moja.

Tangu alipoondoka Liverpool mwaka 2010, Benitez amezifundisha timu za Inter Milan, Chelsea, Napoli, Real Madrid, Newcastle, na Ligi Kuu ya China katika timu ya Dalian Professional.

Baada ya kutambulishwa, kocha huyo alisema: "Nina imani kubwa ya kufanya vizuri na hii klabu inaelekea vizuri, nina shauku kubwa ya kuwa sehemu kubwa ya kuisaidia timu hii kufikia mafanikio."

# Nuno asaini miaka miwili kuinoa Spurs

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur imemteua bosi wa zamani wa Wolves, Nuno Espirito Santo, kuwa kocha wao mpya kwa mkataba wa miaka miwili.

Nuno aliondoka Wolves Mei baada ya misimu minne ya kufanya vizuri, wakati huo alipochukua klabu na kuipeleka robo fainali ya Ligi ya Europa.

Spurs ilimtimua Jose Mourinho Aprili na nafasi yake kuchukuliwa na Ryan Mason mwenye umri wa miaka 29 hadi mwishoni mwa msimu uliopita.

"Ni raha kubwa na heshima kuwa hapa Spurs. Nina furaha na ninatarajia kuanza kazi," alisema Nuno akiwaambia waandishi wa habari wakati akitambulishwa na klabu hiyo.

"Hatuna siku za kupoteza na lazima tuanze kufanya kazi mara moja kabla ya msimu kuanza katika siku chache."

Nuno hatasubiri sana kukutana na klabu yake ya zamani kwani Spurs wana safari ya kwenda kule Molineux kumenyana na Wolves kwenye mchezo wao wa pili wa Ligi Kuu England Agosri 22, mwaka huu.



# DONDOO … OKA
## MAGAZET … LAYA




# ARSENAL YAIFUNIKA JUVE MBIO SAINI YA LOCATELLI

## Miamba ya Hispania, Real Madrid na Atletico pia imehusishwa naye lakini...

**LONDON,** England

ARSENAL wametoa ofa kwa ajili ya kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Italia, Manuel Locatelli na wanaongoza katika mbio za kuwania saini yake, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Sassuolo, Giovanni Carnevali.

**Kiungo wa Sassuolo, Locatelli mwenye umri wa miaka 23, ameonyesha kiwango cha kuvutia kwenye Euro 2020, na alifunga mabao mawili kwa Italia katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Uswisi na kuwasaidia 'Azzurri' hao kufuzu robo fainali.**

Kiwango cha Locatelli kimekuwa bora zaidi kwa msimu wa 2020-21 akiwa na Sassuolo ambao walimaliza nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na hivyo Carnevali amethibitisha Arsenal na Juventus zinamwania kwa udi na uvumba.

"Juventus ni klabu pekee ya nchini Italia ambayo imezungumza kuhusu Locatelli," alisema Carnevali akiiambia Sky Sport Italia.

"Wanania, tumezungumza na Mkurugenzi (Federico) Cherubini wiki iliyopita. "Bado hatutazungumza kuhusu mambo ya kifedha, lakini tuna uhusiano mzuri na tutazungumza haraka hivi karibuni.

"Ni kwamba kuna klabu za kutoka nje zimeonyesha nia ya kumtaka ikiwamo Arsenal, na hadi sasa wao ndio wanaongoza kwenye mbio za kumwania na ndio klabu pekee iliyotoa ofa kwa Manuel."

Miamba ya Hispania, Real Madrid na Atletico Madrid pia imehusishwa na Locatelli, ambaye alionyesha nia ya kutaka kujiunga na Juventus msimu uliopita.

Carnevali aliongeza: "Tunajaribu kumfanya awe mtulivu, hivyo sijazungumza na yeye wala wakala wake bado. Tunaweza kuzungumza kuhusu majaliwa ya Locatelli, lakini juu ya yote kwa sasa anaiwakilisha Italia kwenye Euro."

Inatarajiwa kwamba, Sassuolo watataka kiasi cha Euro milioni 50 ili kumuachia mchezaji huyo zao la AC Milan, ambaye alijiunga na Sassuolo kwa mkopo mwaka 2018 kabla ya kusaini mkataba wa kudumu mwaka 2019.

## ZISIKUPITE

### SANCHO KUPEWA NAMBA 7

JADON Sancho, 22, ambaye amefikia makubaliano kutua Manchester United, atapewa jezi namba saba ambayo kwa sasa inavaliwa na mshambuliaji wa Uruguay, Edinson Cavani, 34. ***(Metro)***

### HAALAND KUTUA CHELSEA

MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich anaamini kwamba 'Blues' hao wanaweza kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland, 20, mwishoni mwa msimu huu. ***(Express)***

### TAVARES HUYO ARSENAL

NYOTA wa Ureno, Nuno Tavares, 21, atafanyiwa uchunguzi wa matibabu katika klabu ya Arsenal kabla ya kujiunga na 'Washikabunduki' hao kwa dau la pauni milioni saba kutoka Benfica. ***(Goal)***

### GORETZKA AWANIWA UNITED

MANCHESTER United pia ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Bayern Munich, Leon Goretzka, 26, ambaye mkataba wake na klabu hiyo ya Bundesliga unakamilika mwaka 2022. ***(Bild)***

### COMAN AOTA MBAWA EPL

KLABU za Manchester United na Liverpool huenda zikashindwa kumsajili Kingsley Coman, wanayemwania baada ya klabu yake ya Bayern Munich kusema anaweza kuuzwa kwa bei ya pauni milioni 77. ***(Bild)***

### CITY KUTETA NA STERLING

MANCHESTER City ina mpango wa kufanya mazungumzo na mshambuliaji wa England, Raheem Sterling, 26, kuhusu hatima yake, huku mchezaji huyo akiwa amesalia na miaka miwili katika mkataba wake na mabingwa hao wa Ligi ya England. ***(Mail)***

### KUMSHAWISHI MBAPPE

RAIS wa Paris St-Germain, Nasser Al-Khelaifi, yupo kwenye harakati za kumshawishi mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 22, kuongeza mkataba wake na klabu hiyo. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo unamalizika mwaka 2022. ***(L'Equipe)***

### UNITED YATAKA NYOTA ZAIDI

WAKATI Manchester United tayari wamefikia makubaliano ya kumsajili winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, sasa wanamwania kiungo wa kati wa West Ham, Declan Rice, 22, beki wa Villareal, 24, Pau Torres na mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane, 27. ***(Guardian)***

### JAMES KUSAJILIWA CHELSEA

CHELSEA wamewasilisha ombi la mwisho kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Lauren James, 19. ***(Goal)***

### BERARDI AGOMBEWA

LEICESTER inakabiliwa na ushindani kutoka kwa AC Milan katika kinyang'aanyiro cha kumsajili winga wa Italia na Sassuolo, Domenico Berardi, 26. ***(Corriere dello Sport)***

# MBUNGE AMBEBA KIDUKU PAMBANO NA MBABE DAR

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

BONDIA Twaha Kiduku, amewaahidi wakazi wa Mkoa wa Morogoro kuwa atamtembezea kichapo mpinzani wake, Dulla Mbabe kwa KO kwenye hatua za awali watakapopanda uliongoni katika pambano lisilo la ubingwa na kunyakuwa zawadi ya gari pamoja na pesa taslimu zinazotarajiwa kutolewa kwa mshindi.

Kiduku alitoa ahadi hiyo mjini Morogoro jana mbele ya Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abdul-Azizi Abood pamoja na wananchi wa manispaa hiyo, wakati wa utambulisho wa mabondia watakaocheza mapambano ya awali.

Akizungumza na wakazi wa Manispaa ya Morogoro walio hudhuria katika utambulisho huo, Kiduku alisema katika pambano lao na Dulla, linalotarajiwa kufanyika Agosti 20, mwaka huu, ameanza kufanya maandalizi ya kutosha na ana uhakika wa kumpiga na kumaliza pambano hilo katika hatua za awali.

"Hapa ni shoo, shoo tu, 'bendera chuma mlingoti chuma', nitampiga Dulla mapema sana, nawahakikishieni Wanamorogoro, gari nitabeba na pesa nitachukua, twendeni Dar es Salaam kwa wingi tukabebe zawadi hizo," alisema Kiduku huku akishangiliwa na wananchi.

Naye Mbunge wa Jimbo la Morogoro, Abood, ameahidi kutoa mabasi mawili bure kwa wakazi wa mkoa wa Morogoro kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya pambano hilo linalofahamika kama "Usiku wa Deni".

Akizungumza wakati wa utambulisho wa mabondia watakaocheza mapambano hayo ya awali, Mbunge huyo alisema ameamua kufanya hivyo ili kuunga mkono juhudi za kukuza mchezo huo.

Mbunge huyo alisema katika kipindi hiki cha maandalizi, atajitolea kwa muda wote ambao Kiduku atakuwa kambini kujiandaa na pambano hilo ili aweza kufanya vizuri na kuleta gari mjini Morogoro.

"Kuanzia leo, nipo tayari kukusaidia kwenye maandalizi yako yote dhidi ya pambano lako na Dulla, lengo langu ninataka ulilete hapa gari kwa maandamano makubwa gari lako mbele mabasi yaliyojaa Wanamorogoro nyuma na maliza pambano mapema si kusubiri kuhesabiwa pointi," alisema Abood.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi wote hasa wakazi wa mkoa huo, kuungana kwa pamoja na kuwasaidia vijana kwenye sekta ya michezo.

Naye Promota wa pambanao hilo, Seleman Semunyu, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Peaktime Media, waandaaji wa pambano hilo, alisema Mbunge huyo ameonyesha njia nzuri kwenye michezo hasa katika Mkoa wa Morogoro.

Alisema kitendo chakusaidia kambi ya Kiduku pamoja nakutoa usafiri ni ishara ya dhamira yake ya dhati ya kusaidia vijana na waandaji wa mchezo wa ngumi.




Bondia Twaha Kiduku (aliyesimama), akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Morogoro jana na kuwahakikishia atampiga Dulla Mbabe kwa KO katika pambano lao linalotarajiwa kufanyika Agosti 20, mwaka huu jijini Dar es Salaam. Waliokaa, aliyevaa miwani ni Mbunge wa Jimbo la Morogoro, Abdul-Aziz Abood na kushoto kwake ni Promota wa pambano hilo, Selemani Semunyu. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Ninja arejea kuivaa Simba SC kesho

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Yanga, Abdallah Shaibu 'Ninja' na Yassin Mustapha, ambao walikuwa majeruhi wa muda mrefu, wameanza rasmi mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi dhidi ya Simba, Jumamosi.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, amesema wachezaji hao wameanza mazoezi baada ya kuwa majeruhi kwa takriban wiki sita.

"Hali ni nzuri, kikosi kinajiandaa vizuri na mazoezi, na habari njema ni kurejea kwa mabeki wetu, Abdallah Shaibu 'Ninja', na Yassin Mustapha, wameungana na wenzao wiki hii, wameanza mazoezi baada ya kuwa majeruhi kwa wiki sita au nane hivi. Kama makocha wetu itawapendeza, basi watakuwa ni sehemu ya kikosi endapo watakuwa fiti. Kama sivyo bado tunao wachezaji ambao wanaweza kuamua mechi hiyo," alisema Bumbuli.

Akizungumzia mechi hiyo, ofisa habari huyo alisema wachezaji wao wanaendelea na mazoezi kujiandaa na mechi hiyo na wataenda kwa kujiamini na kama waamuzi watachezesha kwa haki, basi wataibuka na ushindi.

"Tunaamini mchezo utakuwa mzuri, nina imani kama waamuzi watachezesha kwa haki, tunaweza kuibuka na ushindi bila kujali majina ya wachezaji hao yanayotakwa. Sisi tunakwenda kwa kujiamini na tunaamini tunakwenda kuchukua pointi tatu," alitamba Bumbuli.

Kwa upande wa Simba yenyewe ina mchezaji mmoja tu ambaye itamkosa, naye ni Jonas Mkude ambaye amesimamishwa kwa utovu wa nidhamu.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu ya Simba, Haji Manara, amesema hakuna majeruhi yeyote kwenye kikosi chao, hivyo benchi la ufundi lina uwanja mpana wa kuchagua kikosi.

## KVZ, Polisi kutifuana nusu fainali FA leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

NUSU fainali ya kwanza ya michuano ya Kombe la Shirikisho Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup, inatarajiwa kupigwa leo Ijumaa ikiwakutanisha maafande wa Polisi dhidi ya KVZ.

Katika mchezo huo unaotarajiwa kuchezwa katika Uwanja wa Amaan majira ya saa 10:00 alasiri, makocha wa timu hizo kila mmoja amejigamba kutinga hatua ya fainali kwa kuibuka na ushindi leo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa timu ya Polisi, Yusuph Sape, alisema kikosi chake kimepata muda wa kutosha wakijiandaa na michuano hiyo, hivyo matumaini yake makubwa ameyaweka katika kuhakikisha timu inatinga fainali.

"Tumepata muda wa kujiandaa vya kutosha kilichobaki ni wachezaji kuhakikisha wanatimiza lengo la kutupeleka fainali, tunajua mchezo utakuwa mgumu kwa kuwa KVZ nao ni wazoefu katika mashindano haya na pia ni bingwa mtetezi wa kombe hili," alisema.

Kwa upande wa Kocha wa KVZ, Sheha Khamis, alisema amejipanga kuhakikisha anatetea taji lake hilo msimu huu, ingawa anajua hautakuwa mchezo mwepesi.

## Kiungo Mzimbabwe asaini Simba Queens

**Na Saada Akida**

SIMBA Queens sasa imefanya kweli baada ya kufanikiwa kunasa saini za nyota wawili, kiungo kutoka Zimbabwe, Danai Bhobho, aliyekuwa akiichezea Klabu ya Mwenezana FC ya nchini humo.

Nyota huyo ameingia mkataba wa miaka miwili pamoja na mshambuliaji Aisha Juma aliyekuwa anakipiga kikosi cha Alliance Girls, ambapo amedumu kwa zaidi ya misimu miwili.

Unakuwa ni usajili watatu kwa Simba Queens ambao ni mabingwa mara mbili wa taji la Ligi Kuu ya Wanawake baada ya Juni 29, mwaka huu kumtambulisha Brenda Chaora kuwa kocha mpya wa viungo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema usajili unaendelea kufanyika kwa ajili ya kujiandaa vizuri kwa mashindano ya kimataifa na kwamba umelenga mahitaji ya timu kulingana na mashindano wanayokwenda kushiriki nchini Kenya.

# Michezo

Ijumaa Julai 2, 2021

Nipashe




Arsenal yaifunika Juve saini ya Locatelli

UKURASA 22

ITAKUWA HIVI...



Kipa wa Simba, Aishi Manula, akiwa mazoezini. Kesho anatarajia kuiongoza timu yake kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Yanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

## Uchaguzi TFF wapingwa mahakamani, Karia aitwa

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam, imepokea kesi ya kupinga uchaguzi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) na imemtaka Rais wake, Wallace Karia, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi na Bodi ya Wadhamini ya Shirikisho hilo kufika mahakamani hapo kujibu hoja za kwa nini mchakato wa uchaguzi huo unaoendelea usisimamishwe.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa TFF, Cliford Ndimbo, alisema ni kweli viongozi hao wameitwa mahakamani na wanatakiwa kufika leo asubuhi na baada ya hapo ndipo itajulikana hatima ya uchaguzi huo. “Ni kweli viongozi hao wameitwa mahakamani, hivyo tusubiri tutajua kitakachoendelea baada ya kesho (leo),” alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Wakili Kiomoni Kibamba, alitangaza uchaguzi huo utafanyika jijini Tanga Agosti 7, mwaka huu na tayari usaili wa wagombea wa nafasi ya Kamati ya Utendaji wameshatangazwa pamoja na urais, ambapo Karia ni mgombea pekee.

# WACHEZAJI SIMBA, YANGA WENYEWE WANASEMAJE?

### Wasikie Manula, Bocco na kauli ya Fei Toto, Mwamnyeto na Mukoko, refa hadharani...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI miamba ya soka nchini, Simba na Yanga ikishuka dimbani kesho kwenye mechi ambayo inaweza kuamua bingwa wa Ligi Kuu Bara, ama kuendelea kumchelewesha, wachezaji wa timu hizo wameizungumzia ‘dabi’ hiyo ya watani wa jadi, twende sasa...

**Mechi hiyo ya mzunguko wa pili itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Saalam majira ya saa 11:00 jioni, Simba ambao ni mabingwa watetezi, watashuka uwanjani hapo wakiwa na lengo moja tu la kushinda ili kutawazwa mabingwa kwa mara ya nne mfululizo.**

Simba kwa sasa ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 73 baada ya mechi 29, hivyo inahitaji ushindi tu ili kutawazwa mabingwa wakati Yanga yenye alama 67 zilizotokana na kushuka dimbani mara 31, ipo nafasi ya pili, hivyo endapo ikishinda itawachelewesha watani wao kutwaa taji hilo.

Lakini mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu zaidi kutokana na ukweli kwamba Yanga haitakubali kuwa daraja la Simba kutangaza ubingwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na mwandishi wetu, wachezaji wa timu hiyo, kila mmoja alikiri mchezo huo kuwa mgumu, lakini wakieleza dhamira ya timu zao kuibuka na ushindi.

Nahodha na mshambuliaji wa Simba, John Bocco, alisema ni mechi kubwa na si tu kwa klabu hizo na wachezaji bali pia kwa nchi nzima kutokana na ushindani uliopo kwa timu hizo mbili.

“Dabi ni dabi, ni mchezo mkubwa kwa nchi katika ligi yetu, ukiangalia ushindani uliopo katika timu hizi ni mkubwa, kwa hiyo ni kitu cha kujivunia sisi kama wachezaji kuwa moja ya watu watakaohusika katika tukio hili. Lakini mwisho wa siku ndiyo kazi yetu tumeajiriwa kwa kazi hii, na uzuri zaidi tunacheza kutafuta pointi ili tuweze kujitangazia ubingwa msimu huu,” alisema Bocco.

Kipa wa Simba, Aishi Manula, alisema: “Tunaenda kuonyesha kile tulichokuwa nacho msimu mzima, ni kwamba tunaenda kucheza mechi ambayo tunaamini tutatangaza ubingwa. Kwetu tunaona ni furaha zaidi kama tutatangaza ubingwa mbele ya watani wetu wa jadi.

“Hivyo kwetu ni fursa kubwa na nadhani ubingwa wetu utashereheshwa vizuri kama tutapata pointi tatu dhidi ya watani wa jadi, ila dabi ni dabi, siku zote, kama unavyoona inaanzia nje ya uwanja na sasa tupo katika wiki ya dabi na tayari nchi imeshagawanyika.”

Beki wa kulia wa timu hiyo, Shomari Kapombe, yeye alisema: Upinzani wetu sisi na wao ni mkubwa na ukiangalia ni kwamba hawatakubali kuona sisi tunatangaza ubingwa mbele yao, lakini tunajipanga kuona tunafanya kitu hicho kwao.”

Wakati wachezaji wa Simba wakieleza lengo lao hilo la kutaka kufanya watani wa jadi kuwa daraja la ubingwa, nyota wa Yanga akiwamo beki wa kati, Bakari Mwamnyeto, alisema: “Maandalizi mpaka sasa yapo vizuri, wachezaji wote wapo salama, benchi lote la ufundi lipo vizuri, maelekezo tunapata vizuri kutoka kwa walimu.

“Tunachoweza kuwaambia mashabiki wetu, waje kwa wingi tarehe 3 (kesho) ushindi upo, wapinzani tumewaangalia udhaifu na uzuri wao na kila siku mazoezi tunayafanyia kazi na walimu wanatuelekeza jinsi ya kucheza nao. Tumejipanga vizuri kuwakabili na tunaweza kupata pointi tatu.”

Kiungo wa timu hiyo, Feisal Salum ‘Fei Toto’, yeye alisema: “Maandalizi kwa sisi wachezaji tupo vizuri, na benchi la ufundi wanaendelea kutupa ujuzi mkubwa. Namshukuru Mungu tupo vizuri, mashabiki wanaokuwapo nyumbani na wanaokuja uwanjani, waje kwa wingi tu, sisi wachezaji wao tumewaandalia zawadi nzuri.”

Kauli hiyo ya Fei Toto na ile ya Mwamnyeto, ziliungwa mkono na winga mshambuliaji wa timu hiyo, Deus Kaseke pamoja na kiungo mkabaji, Mukoko Tonombe ambao walisema kilichobaki ni kuendelea na maandalizi kwa ajili ya mchezo huo wa kesho huku wakiwataka mashabiki wa Yanga kujitokeza kwa wingi uwanjani kesho.

Wakati huo huo, Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), imemtangaza Emmanuel Mwandembwa kutoka Arusha kuwa mwamuzi wa kati katika mechi hiyo huku akisaidiwa na Frank Komba (Dar) na Hamdan Saidi (Mtwara).


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >